KIELELEZO CHA KIBIBLIA KWA

# MAFUNZO YA VIONGOZI WA KANISA



na

Roy T. Edgemon na Arthur H. Criscoe

7. Tumia dakika chache kufanya marudio na kufikiria masomo yote. Waongoze washiriki kushirikiana wazi kuhusu jinsi watakavyojibu maswali haya mawili:

Je, wazo kuu ambalo umelishika zaidi kutokana mafundisho haya ni lipi?

Je, sasa umeamua kufanya nini kufuata mkazo wa masomo yako?

8. Toa shukrani zako kwa washiriki waliokuwa waaminifu katika masomo haya. Soma pamoja kwa sauti Mithali 3:5-6.

9. Hakikisha unazo rekodi zote za kozi hii. Ikiwa itahesabiwa kama kozi kwa T.E.E. toa taarifa washiriki wapatie kibali.





# KIELELEZO CHA KIBIBLIA KWA MAFUNZO YA VIONGOZI WA KANISA

**Waandishi: Roy T. Edgemon na Arthur H. Criscoe**

Mfasiri: J. K. Kiimbila

Mhariri: Betty Ann Whitson

Kutoka muswada wa kitabu: A Biblical Model for Training Leaders

Kiswahili Edition
Published and ©Copyrighted by
Baptist Publications House
Thika Road, Ruaraka
P.O. Box 30370, Nairobi, Kenya

## DIBAJI

Mwezi wa Julai, 1982 Warsha ya Elimu ya Kikristo ya Kamati ya Uinjilisti na Elimu ya Baptist World Alliance ilikutana Nairobi, Kenya. Washiriki wa warsha hiyo walijadiliana haja ya kuwasaidia wachungaji wa Kibatisti duniani kote kwa kujenga maktaba ya msingi ya vitabu vya theolojia na mafundisho ya huduma.

Mchungaji kutoka Uganda akivalia mavazi rasmi ya nchi yake alisimama. na kusema. Alipoanza kuzungumza, ilikuwa wazi kwamba uso wake ulikunjamana kutokana na huduma ya kujitoa wakati wa mateso na shida. Tulisikiliza kwa makini sana. Kwa kirefu na kwa ufasaha alitoa maombi ya kupatiwa vitabu kwa ajili ya wachungaji wenzake wanaotumika katika sehemu zenye taabu katika shamba la mizabibu ya Bwana.

Kijitabu hiki cha mwongozo kimeandikwa kwa ajili ya ndugu mchungaji kutoka Uganda na kwa ajili ya wachungaji wenzake kote duniani. Tunaamini kwamba kitatumiwa kama maandishi mafupi na ya msingi kuhusu uongozi wa Kikristo. Aidha kitatoa mwongozo kuhusu utakavyowafundisha viongozi katika kanisa lako.

Watu wengi wenye uzoefu mbalimbali wamechangia mitazamo ya waandishi na kuelewa vema kuhusu uongozi wa Kikristo. Tuna toa shukrani kwa wote waliosaidia kujenga mawazo yetu. Baadhi ya masomo katika kijitabu hiki yamerekebishwa kutoka kitabu *Youth Becoming Leaders* kilichoandikwa na Arthur H. Criscoe (Convention Press, 1985). Maandiko Matakatifu yote ya Biblia yametolewa kutoka Biblia ya Kiswahili (United Bible Societies 1952). Waandishi wanatoa shukrani kwa Bodi ya Wabatisti ya Shule ya Jumapili, Southern Baptist Convention, kwa ajili ya kuunga mkono kwa dhati na kujitoa kabisa kwa mafundisho ya viongozi. Bila ya msaada wao, kijitabu hiki cha mwongozo kisingewezekana kuandikwa.

## SOMO LA TANO

*HATUA SABA KATIKA MAFUNZO YA KIONGOZI MTUMISHI*

### Sura 5 na 6

**Shabaha**: Baada ya kumaliza somo hili, washiriki wangeweza:

1. Kujumlisha kazi ya mchungaji kama mkamilishaji ndani ya kanisa lake.
2. Kueleza kwa kifupi jinsi ya kugundua mahitaji ya mafunzo katika kanisa.
3. Kutaja angalau mafunzo matatu ambayo yangekuwa ni sehemu ya kuwafunza viongozi watumishi.

### Kabla ya Mjadala

1. Andaa fundisho fupi juu ya "Wajibu wa Mchungaji kama Mkamilishaji" kutoka Sura 6.
2. Andaa fundisho fupi juu ya sehemu nane za masomo. Zinapaswa ziwe chini ya "Mafunzo ya Jumla", ukarasa 47-51
3. Andika kwenye vipande virefu vya karatasi sehemu hizi nane.

### Wakati wa Mjadala

1. Tumia Kadi yenye orodha ya masomo na kurudia masomo yote. Soma msingi wenye sehemu tatu kuhusu mpango wa kuwafunza viongozi, ukurasa. 46 chini ya "Maelezo kwa Jumla".
2. Fundisha kwa kifupi "Wajibu wa Mchungaji kama Mkamilishaji" na acha nafasi ya majadiliano.
3. Fundisha kwa kifupi juu ya sehemu nane za masomo zinapaswa ziwe katika mafunzo ya viongozi. Weka karatasi na sehemu ubaoni unapotoa maelezo juu yake.
4. Angalia maandiko juu ya Mafunzo wakati wa Kazi, ukarasa 47. Waulize washiriki ikiwa wamejifunza kazi wanazofanya kwa kufunzwa wakati wa kazi. Zungumza jinsi mafunzo wakati wa kazi yanavyoweza kulisaidia kanisa.
5. Waongoze katika majadiliano juu ya umuhimu wa kuwa na mfano na kielelezo kizuri (Sura 6). Waulize wawili watatu kushirikisha majibu yao katika zoezi, ukurasa 65.
6. Jadili "Mambo ya Kuwazia", ukurasa 63.

## SOMO LA NNE

*KUMTAYARISHA KIONGOZI MTUMISHI*

## Sura 4

**Shabaha**: Baada ya kumaliza kipindi hiki, washiriki wangeelewa zaidi juu ya sifa za viongozi watumishi. Washiriki wataweza:

1. Kutaja angalau sifa tano zinazoonekana ndani ya viongozi watumishi.
2. Kutambua tabia moja katika maisha yao ambako marekebisho yanahitajika.
3. Kuorodhesha asili nne za uwezo kwa kiongozi mtumishi.

## Kabla ya Mjadala

1. Mwulize mtu mmoja kuleta taarifa juu ya "Maisha ya Kiroho ya Kiongozi Mtumishi". Mkumbushe kukaza asili nne za uwezo.

## Wakati wa Mjadala

1. Waulize washiriki kuangalia "Sifa za Viongozi Watumishi" kuanzia ukurasa 36-38. Waombe kujipima wao wenyewe unaposoma sifa na maelezo yake kwa kufuata mizani upande wa kulia.
2. Tumia dakika chache kumaliza kazi ya kufanya, ukurasa·37
3. Angalia "Tao la Uongozi wa Kitumishi". Waulize watu kusoma chati linalofuata "Tao" na wape washiriki nafasi ya kujipima maisha yao sifa inaposomwa. Acha nafasi ya mazungumzo.
4. Wagawe washiriki kwenye makundi mawili na wape maandiko ya kusoma chini ya "Uongozi wa Kitumishi katika Matendo". Wape nafasi kupeana mawazo na halafu waombe kwa taarifa zao.
5. Mwulize mshiriki kutoa taarifa fupi juu ya "Maisha ya Kiroho ya Kiongozi Mtumishi". Toa nafasi ya mazungumzo.
6. Waulize washiriki kukamilisha zoezi la kujitambua kwenye ukurasa wa 39 Waulize baadhi ya washiriki kushiriki sehemu zenye nguvu na zile zenye udhaifu za maisha yao.
7. Funga mkutano kwa kusoma "Muhtasari" kwenye ukurasa wa 44.



## YALIYOMO

Sura ya 1: HAJA YA KUWA NA VIONGOZI . . . . . . . . . . 5
Haja ni Kubwa
Mungu Amemgawia Kila Mtu
Malengo ya Kujifunza
Maelezo kwa Jumla

Sura ya 2: MTAZAMO YA KIBIBLIA KUHUSU UONGOZI . . . . . . . . . . 8
Maelezo kwa Jumla
Mawazo ya Kidunia Kuhusu Uongozi
Utumishi Ndio Siri
Yesu Ndiye Kielelezo Chetu
Mafundisho Mengine ya Kibiblia Kuhusu Utumishi

Sura ya 3: KARAMA ZA UONGOZI WA KITUMISHI . . . . . . . . . . 22
Maelezo kwa Jumla
Karama za Kiroho ni Nini
Kweli Nane za Kibiblia Kuhusu Karama za Kiroho
Namna ya Kugundua Karama Zako

Sura ya 4: MPANGO WA KUWAFUNZA VIONGOZI WATUMISHI . . . . . . . 34
Maelezo kwa Jumla
Kuwatafuta Watakaokuwa Viongozi Watumishi
Sifa za Viongozi Watumishi
Uongozi wa Kitumishi katika Matendo
Maisha ya Kiroho ya Kiongozi Mtumishi

Sura ya 5: HATUA SABA KATIKA MAFUNZO YA KIONGOZI. . . . . . . . . . .45
Maelezo kwa Jumla
Gundua Mahitaji
Panga Mambo kwa Kufuata Umuhimu Wake
Chagua Yatakayofundishwa na Taratibu za Kuifuata
Mafunzo ya Jumla
Mafunzo Maalumu
Mafunzo Wakati wa Kazi
Orodhesha Viongozi Wanaonekana Watafaa
Endesha Mafunzo
Watambue Unaowafunza
Fuatilia

Sura ya 6: UONGOZI WA UCHUNGAJI NA WAJIBU . . . . . . . . . . 58
Maelezo kwa Jumla
Wajibu wa Mchungaji kama Mkamilishaji
Umuhimu wa Mchungaji kama Kielelezo

Mwongozo kwa Semina Kuwafunza Viongozi wa Kanisa Lako . . . . . . . . . 64

## UTANGULIZI

Unakaribishwa kusoma *Kielelezo cha Kibiblia kwa Mafundisho ya Viongozi wa Kanisa*. Kama unahusika na kuwafundisha viongozi kwa ajili ya kanisa lako, basi kijitabu hiki cha mwongozo ni kwa ajili yako. Kabla hujaanza masomo yako, tunataka kukueleza kwa kifupi mwongozo uliyotumika katika kijitabu hiki.

Utafanya mazoezi ya kujifunza wakati unaposoma kijitabu hiki. Wataalamu wa elimu wamekuwa wakituambia kwa muda mrefu kwamba watu hujifunza zaidi wanapofanya mazoezi wakati wanapofunza. Sote tunajua kutokana na uzoefu ya kwamba hii ni kweli. Labda unakumbuka wakati ulipogusa stovu ya moto mkali au ulipoponda kidole chako na nyundo na ukajifunza kutokana na uzoefu huo ambao haujausahau. Tunajifunza kwa kutenda. Methali ya Kichina inaeleza ukweli huu: "*Nasikia* **na nashangaa;** *Naona* **na nakumbuka;** *Natenda* **na naelewa.**"

Kijitabu hiki kimetayarishwa ili wewe uyatafakari masomo wakati unapofanya mazoezi. Usisite kuandika katika kijitabu hiki unapoambiwa kujaza katika nafasi iliyo wazi au kuandika jibu lako chukua kalamu yako na kufanya hivyo. Kwa njia hii, utajifunza zaidi kuliko kujifunza kwa kusoma tu.

Unatakiwa uwe na Biblia yako karibu nawe unapofanya mazoezi ya kijitabu hiki. Mara kwa mara utaombwa kuchukua Biblia yako na kusoma kifungu fulani. Hakikisha kwamba unafanya hivyo bila kukosa, kwani hii ni sehemu muhimu ya mafundisho yote. Ni muhimu sana kusikia Mungu anasema nini kuhusu mafundisho ya viongozi.

Kijitabu hiki cha mwongozo kinakuwezesha kujifunza kutokana na muda wako na saa zinazokufaa. Ni juu yako kujifunza kwa haraka au polepole unavyotaka. Hata hivyo, utakuwa na maendeleo mazuri ya kujifunza na kuyaimarisha ikiwa husomi kwa kupitia pitia.

Tunashauri kwamba umalize sura mbili kila juma. Kwa njia hii utamaliza masomo yote kwa muda wa majuma matatu. Baadaye utakapokuwa unawafundisha watakaokuwa viongozi katika kanisa lako, utahitaji kusoma tena masomo haya.

Unatakiwa uchague wakati wako unaofaa na mahali pa kujifunzia. Tunapendekeza kwamba utafute mahali pa kimya ambapo unaweza kujifunzia bila ya kuingiliwa. Anza kila kipindi cha kujifunza na sala. Mwombe Mungu akuwezeshe kujifunza kwako kuwe na maana. Pia tunaomba kwamba kujifunza kwako kutakuwezesha uwafundishwe viongozi zaidi kwa ajili ya kanisa lako.

Methali nyingine ya Kichina inasema: "Safari ya maili elfu moja huanza na hatua ya kwanza". Methali ya Kimarekani yenye maana kama hiyo inasema: "Njia bora zaidi ya kukamilisha jambo ni kuanza". Haya anza!

3. Andaa fundisho fupi juu ya 'Kweli Nane za Kibiblia kuhusu Vipawa vya Kiroho".

4. Andaa fundisho fupi kuhusu "Jinsi ya Kuwasaidia Washiriki wa kanisa kugundua Karama Zao".

### Wakati wa Mjadala

1. Andika maana ya "karama ya kiroho" ubaoni. Waongoze washiriki kutafuta karama zinazotajwa katika Warumi 12:6-8; 1 Wakorintho 12:8-10 na 28-30; na Waefeso 4:11. Usisahau kuwaambia kwamba watu wengi wafikiri hizi zinazotajwa hapa ni mifano wa baadhi ya karama. Siyo orodha ya karama zote. Orodhesha karama ubaoni zinazotajwa.

2. Rudia "Chati ya Karama" Sura 3. Waulize watu mbalimbali kusoma karama hizi pamoja na maelezo. Waulize washiriki kutaja watu fulani na karama zinazoonekana katika maisha yao. Waelezee maoni matatu kuhusu karama za "alama".

3. Wagawe washiriki katika makundi madogo matatu. Angalia orodha ya vifungu vya Biblia na watu kwenye ukarasa 25. Kundi la kwanza litachunguza maandiko kutoka numbari 1 hadi 3; kundi la pili kutoka numbari 4-6; na kundi la mwisho kutoka numbari 7- 9. Kila kundi liwe tayari na majibu kuhusu watu na karama zao.

4. Fundisha kwa kifupi juu ya "Kweli Nane za Biblia kuhusu Karama za Kiroho". Waonyesha kweli hizi ambazo umesha andika kwenye kadi unapofundisha. Acha nafasi kwa majadiliano.

5. Soma maswali yanayoandikwa kwenye ukurasa 31 na wape washiriki nafasi kwa mazungumzo.

6. Fundisha juu ya maandiko "Namna ya kuwaongoza washiriki wa kanisa lako kugundua karama zao". Kwa kila pendekezo unayofundisha, weka karatasi yake ubaoni. Wahusishe washiriki katika majadiliano waongoze kutoa mawazo juu ya mapendeleo yao.

7. Uwe na wakati wa kuwaongoza washiriki kusaidiana katika kutambua karama zao. Weka mshiriki mmoja kuketi kimya wengine wanapotoa mawazo yao kuhusu karama zake. Wanaweza kusema:

"Uwezo mmoja ninaouona katika maisho yako ni ...."; "Karama inayoonekana ndani yako ni ..." Ikiwa kundi lako ni kubwa mno, wagawe washiriki katika makundi madogo ili kila mmoja awe na nafasi kuyasikia maoni ya wenzake.

8. Funga mafundisho kwa kupeana mikono mtu na mwenzake na kuomba ombi la kumshukuru Mungu kwa wema yake.

1. Wakaribishe washiriki. Shiriki katika shabaha za somo hilo. Mwulize mmoja kufungua mafundisho na maombi.

2. Kuanzia na Luka 22:24:27, rudia maandiko kumi yanayohusu mafundisho ya Yesu juu ya utumishi. Tumia wakati wa kutosha kusoma kila andiko na kuwaongoza washiriki kutaja fundisho kuu kuhusu utumishi kutoka kwake. Kisha uwaongoze washiriki kuzungumza jinsi mafundisho haya yanavyoweza kutumiwa katika maisha yao siku hizi.

3. Fundisha kwa kifupi juu ya tendo la Yesu akitawadha miguu ya wanafunzi wake. Mwulize mmoja asome Yohana 13:1-17.

4. Mwulize mtu uliompa kazi kutoa taarifa yake juu ya "Paulo kama Kiongozi".

5. Mwulize mmoja kusoma 1 Petro 5:1-7. Kisha waongoze wayajibu maswali manne kwenye ukurasa 22.

6. Weka kadi ndogondogo yenye majina ubaoni/ukutani. Waulize washiriki kueleza tabia za watu hawa zinazowaonyesha kuwa viongozi watumishi.

7. Soma maneno yanayoeleza kuhusu utumishi kuanzia usemi "Njia ya kuwa mkubwa ni kuwa mtumishi". Waulize washiriki kufikiria mifano mizuri ya hizi: "Njia ya kupokea ni kutoa", "Njia ya kupata ni kupoteza" na "Njia ya kuishi ni kufa".

8. Funga mafundisho kwa kusisitiza "Muhtasari" wa Sura 2.

## SOMO LA TATU

*KIPAWA CHA MTUMISHI WA UONGOZI*

### Sura 3

**Shabaha**: Baada ya kumaliza kipindi hiki washiriki wangeelewa zaidi kuhusu karama za kiroho. Wataweza:

1. Kujumlisha mafundisho ya Biblia juu ya karama za kiroho.
2. Kutambua karama mbalimbali ndani ya maisha ya wengine.
3. Kueleza jinsi mtu mwingine anavyoweza kutambua karama zake za kiroho.

### Kabla ya Mjadala

1. Andika ubaoni kweli nane za karama za kiroho.

2. Andika kwenye vipande virefu vya karatasi hatua sita za kuwasaidia washiriki wa kanisa lako kugundua karama zao.



## SURA YA 1

# HAJA YA KUWA NA VIONGOZI WA KIKRISTO

### Maelezo kwa Jumla

Sura hii inatoa utangulizi wa kijitabu hiki cha mwongozo na inaeleza malengo ya mafunzo wakati ukijifunza. Sura ya pili inakuonyesha mtazamo wa Kibiblia juu ya uongozi, ambao ni kutumikia wengine, utumishi. Karama za kiroho zinaelezwa katika sura ya tatu. Sura ya nne inataja sifa za viongozi na inatilia mkazo maisha ya kiroho ya kiongozi.

Sura ya tano inaeleza hatua kwa hatua mpango wa kuwafunza viongozi. Sura hii pia ina mafunzo ya vitendo na ya kimsingi yaliyo sehemu ya lazima katika mafunzo ya viongozi. Sura ya sita inahusu wajibu wa mchungaji katika kuwafunza viongozi.

### Haja ni Kubwa

Haja ya kuwa na viongozi wa Kikristo ni kubwa.Kama kanisa lako ni kanisa liliokamilika kama mengine, unahitajika kulichunguza na kuona kama kuna haja kubwa ya kuwa na viongozi. Makanisa mengi yana vikundi viwili: (1) Kundi kubwa la "watazamaji" wanaohudhuria ibada za Jumapili na (2) Mchungaji pamoja na watu wachache wanaofanya karibu shughuli zote. Jambo hili halipatani na mafundisho ya Biblia. Mungu hakukusudia mchungaji afanye kazi zote za huduma kwa ajili ya kanisa. Haiwezekani mtu mmoja kufanya hivyo. Mungu anataka kila mmoja ajihusishe katika huduma za kanisani.

Hebu tumia muda kidogo, fikiria juu ya kanisa lako. Zingatia hitaji lako la kuwa na viongozi. Na jibu maswali yafuatayo:

1. Kuna watu wangapi kanisani mwako wanaojihusisha na kazi za uongozi?
2. Kuna watu wangapi kanisani mwako wanaojihusisha hasa katika aina fulani ya huduma ya kanisa?
3. Ni shughuli zipi unazofanya zinazopashwa kufanywa na viongozi wa kujitolea kanisani mwako?
4. Pangetokeamabadiliko gani kanisani mwako nakatikajumuiya kamakilamshirikiwa kanisa lako angejishughulisha katika huduma?

Sasa, orodhesha hapa chini shughuli muhimu zinzaohitaji viongozi katika

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

## Mungu Amemgawia Kila Mtu

Kila Mkristo ana karama. Akiwa ni mwanamume au mwanamke amepewa karama za kiroho. Soma Waefeso 4:7-8 na 1 Wakorintho 12 ukaone ukweli huu unavyotajwa waziwazi katika Biblia. Biblia pia inafundisha kwamba kila Mkristo ni mhudumu, yaani mtumishi. Soma Waefeso 4:11-12. Ukweli huu ni kiini cha mafundisho ya Agano Jipya kuhusu ukuhani wa waumini wote. Kila mwaumini anapaswa kujihusisha katika kazi za huduma akitumia karama na uwezo (talanta) wake. Matokeo ya jumla ya kujifunza masomo ya kijitabu hiki yatakuwa kwamba kanisa lako litajihusisha kwa vitendo katika huduma ya Kristo. Kwenye jumuiya yako na duniani kote watu lazima waletwe kwa Kristo, Wakristo wakomae kama wanafunzi wa Yesu na watu wahudumiwe mahitaji yao. Kwa njia hiyo, kazi yako kama mchungaji itakuwa rahisi zaidi na yenye kuridhisha zaidi wakati Wakristo wengine watakapokamilishwa kutumikia wakiwa viongozi na wakisaidia katika wajibu wa uongozi.

Sasa, kutokana na mahitaji ya uongozi kanisani mwako na kuelewa kwako yaliyomo katika kijitabu hiki, unategemea kijitabu hiki kitakusaidiaje? Andika mambo matatu au manne unayotegemea kupata kutokana na masomo haya.

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________



kwa neno moja mbili. Kisha toa muhtasari wa maandiko chini ya "Utumishi ndio Ufunguo", Sura 2.

9. Wagawe washiriki katika makundi mawili. Waulize kusoma Waefeso 2: 5-11. Kundi moja lijibu "Yesu yu Nani". Kundi la pili lijibu "Yesu alifanya nini". Tumia dakika chache, halafu waite kwa taarifa zao.

10. Waulize washiriki wote kufungua Biblia na kusoma Luka 4:18-30 na kutazama kwa matendo matano Yesu alikuja ulimwenguni kufanya. Orodhesha kwenye ubao/karatasi. Kisha waulize tuona vyo katika huduma ya Yesu kutuonyesha kazi ya kiongozi mtumishi?

11. Waulize wale watatu kutoa taarifa zao juu ya Isaiah 42:1-7.

12. Funga na maombi.

## SOMO LA PILI

*MTAZAMO WA KIBIBLIA JUU YA UONGOZI, SEHEMU 2*

## Sura 2

**Shabaha**: Baada ya kumaliza somo hilo, washiriki wangeelewa bora mtazamo wa Kibiblia juu ya uongozi. Wataweza:

1. Kujumlisha mafundisho ya Yesu juu ya uongozi utumishi.

2. Kusema Paulo alikuwa kiongozi wa namna gani.

3. Kueleza mafundisho ya Petro juu ya uongozi utumishi.

4. Kutaja angalau watu watano zaidi kutoka katika Biblia walioku wa viongozi watumishi.

### Kabla ya Mjadala

1. Andaa fundisho fupi juu ya Yohana 13:1-17.(Yesu akitawadhaa miguu ya wanafunzi wake). Rudia masomo kutoka Sura 2.

2. Mwulize mtu mmoja alete taarifa fupi kuhusu "Paulo kama Kiongozi" akitumia mawazo kutoka Sura 2.

3. Andika majina haya kwenye kadi ndogondogo: Musa, Yoshua, Eliya, Isaya, Yeremia, Amosi, Yona, Danieli, Abrahamu, Kalebu Ayubu, Daudi, Hezekia, Yakobo, Yohana, Yuda, Fibi, Epafra.

### Wakati wa Mjadala

## SOMO LA KWANZA

*MTAZAMO WA KIBIBLIA JUU YA UONGOZI, SEHEMU YA KWANZA Utangulizi na Sura za 1 na 2*

**Shabaha**: Baada ya kumaliza kipindi hiki washiriki wangeelewa zaidi mafundisho ya Biblia juu ya uongozi. Wataweza 1) Kutambua kichwa kikuu cha uongozi wa Kikristo, 2) Kueleza katika maneno yao Yesu alikuuwa kiongozi wa aina gani wakati wa huduma yake duniani.

### Kabla ya Mjadala

1. Uwe na nakala za kitabu hiki za kutosha kwa ajili ya wale ambao hawakupata zao. Weka kitabu cha kuwaandikisha wanaohudhuria.

2. Andaa fundisho fupi juu ya "Mungu Amemgawia Kila Mtu". Tumia vifungu kutoka katika Waefeso 4:7-8; 1 Wakorintho 12 na Sura 1 ya kitabu hiki.

3. Waulize watu watatu kutoa mawazo yao mafupi juu ya Isaya 42: 1-7. Wasome vifungu hivi kwa Sura 2. Mmoja atoe mawazo juu ya 1) "Uhusiano wake Isaya na Mungu"; wa pili "Msimamo na mwenendo wake Isaya", na wa tatu 3) "Mtumishi wake Isaya".

### Wakati wa Mjadala

1. Wasalimie washiriki. Andika majina kwenye orodha. Watambulishe wageni na hakikisha wote wanavyo vitabu vyao. Sisitiza umuhimu wa kujibu maswali yote.

2. Tangulia kwa kuonyesha kadi na kusoma visa vya masomo yote. Fungua na maombi kumwomba Mungu abariki kila mmoja.

3. Ongoza majadiliano mafupi juu ya haja ya viongozi, kutumia maandiko kutoka Sura 1. Uliza maswali yanayoorodheshwa chini ya "Haja ni Kubwa".

4. Waulize watu wawili kusoma Waefeso 4:7-8 na 1 Wakorintho 12. Toa fundisho uliloandaa kuhusu "Mungu Amemgawia Kila Mtu".

5. Shiriki katika shabaha zote tatu za kitabu hiki (ukarasa 7). Halafu kaza shabaha za somo hilo.

6. Tumia dakika chache kujadili juu ya "Mambo ya Kuwazia" mwisho wa Sura 1.

7. Uliza swali: Mtazamo wa dunia juu ya uongozi ni nini? Waulize kutazama kwenye maandiko ya Sura 2 na jadili kwa kifupi juu ya jibu.

8. Andika ubaoni au kwenye karatasi maneno "mtumishi" na "mtumwa". Waulize wafikirije wanapowaza juu ya maneno haya. Orodhesha mawazo yao



### Muhtasari

Ufuatao ni muhtasari mfupi wa sura hii:

1. Kuna haja ya kuwa na viongozi katika kila kanisa.

2. Kila Mkristo amepewa karama za kiroho na kila Mkristo ni mhudumu.

3. Malengo makuu ya kijitabu hiki ni kwamba utaelewa vizuri zaidi mtazamo ya Kibiblia juu ya uongozi na ya kwamba utaweza kufuata mpango wa hatua kwa hatua katika kuwafunza viongozi wa baadaye.

4. Kiini cha kijitabu hiki ni mtazamo ya Kibiblia juu ya uongozi, yaani utumishi.

### Mambo ya Kuwazia

Hebu fikiria kwa dakika chache sura hii itakuwa na manufaa gani katika kuwafunza viongozi kanisani mwako.

- Sehemu kubwa katika kanisa langu viongozi wanaohitajiwa ni ______

______

- Sababu mojawapo kwa nini washiriki kanisani mwangu hawaelewi kikamilifu ukweli wa Biblia ya kwamba kila Mkristo ni mhudumu pengine ni ______

______

______

- Mambo ambayo ningependa kuona yanatokea kanisani mwangu katika sehemu ya mafunzo ya uongozi ni haya hapa: ______

______

______

______

______

______

______

## SURA YA 2

# MTAZAMO WA KIBIBLIA JUU YA UONGOZI

## Maelezo kwa Jumla

Kusudi la sura hii ni rahisi, kama utawafunza viongozi kwa ajili ya kanisa lako, basi wataka kuwafunza ili wawe viongozi wanaofaa. Utawataka waelewe mtazamo wa Kibiblia juu ya uongozi. Sura hii (1) inaeleza mtazamo wa Kibiblia juu ya uongozi, ikitofautiana na mtazamo wa kidunia; (2)inaonyesha yale Yesu aliyoyafundisha kuhusu utumishi na alivyotoa mfano wa utumishi; na (3) inatoa mifano mingine ya uongozi wa kitumishi katika Biblia.

## Mawazo ya Kidunia kuhusu Uongozi

Njia ya kidunia na njia ya Mungu ni tofauti. Tofauti hii inaonekana wazi wazi katika jambo linalohusu uongozi. Dunia ina mawazo yasiyo sahihi kuhusu uongozi.

Mtazamo wa kidunia juu ya uongozi ni ule ya mtu mmoja akiwasimamia watu wengine na akitumia mamlaka na uwezo wake. Mara nyingi kiongozi ni mtu aliye na kipaji cha pekee, mamlaka na uwezo wa kuamrisha. Ama ni mtu mwenye akili ya kiwango cha juu na ubunifu au mtu mwenye ustadi usio wa kawaida au hadhi inoyowavutia watu.

Mitazamo ya kidunia juu ya uongozi siyo ya Kibiblia. Kuna tofauti ya kimsingi kati ya uongozi unavyotumiwa duniani na uongozi unavyo tumiwa na watu wa Mungu. Yesu alisema jambo hili kwa mkazo, "Mwajua ya kuwa wakuu wa mataifa huwatawala kwa nguvu, na wakubwa wao huwatumikisha. Lakini haitakuwa hivyo kwenu, bali mtu ye yote anayetaka kuwa mkubwa kwenu, na awe mtumishi wenu." (Mathayo 20:25-26).

## Utumishi Ndio Ufunguo

Yesu Kristo ni kielelezo bora cha uongozi kuliko vyote duniani. Yesu ni kiongozi Mkamilifu. Kwa kweli, yeye ndiye kiongozi mkamilifu pekee. Kujifunza maisha yake na mafundisho yake ili kuelewa uongozi, ni kujenga msingi imara wa uongozi wa Kibiblia.

Yesu alitenda na kufundisha akipinga mtazamo wa kidunia juu ya ukubwa na uongozi. Alieleza kwa muhtasari na kwa nguvu sana, "Bali mtu anayetaka kuwa mkubwa kwenu, atakuwa mtumishi wenu, na mtu anayetaka kuwa wa kwanza wenu, atakuwa mtumwa wa wote."(Marko 10:43-44).

Yesu alitumia maneno mawili maalum katika kifungu hiki kueleza maana ya neno "uongozi". Neno la kwanza, linalotumiwa katika mstari wa 43 ni



4. Jifunze kijitabu hiki na maliza kazi zote za kufanya kabla hujaanza masomo haya.

5. Kusanya vifaa utakavyohitaji kwa mafundisho. (vitabu, kara tasi, ubao, chaki, kalamu, nk.)

6. Tengeneza fomu za kuwaandikisha wanafunzi. Pengine somo hilo linaweza kuhesabiwa na T.E.E.

### Hatua za Kupanga Mjadala

1. Soma na kujifunza sura utakazofundisha kwa uangalifu. Fuata mapendekezo kwa kufundisha sura zile. Jibu maswali na amua yale utakayotumia. Andika njia utakazofuata kuwasaidia wana funzi na kuwavuta.

2. Weka tayari vifaa vyote utakavyohitaji kwa somo hilo.

3. Toa kazi kwa watu kadhaa mapema. Hakikisha kila mmoja anaelewa kazi yake ya kufanya.

4.Andaa mahali pa kukutanikia pawe pazuri na pa usikivu kwa kujifunza.

5. Wahi kwa kila somo kuwakaribisha washiriki na kuongea nao. Anza na malizia kwa saa iliyopangwa.

6. Wakumbushe wanafunzi kuleta Biblia zao na kumaliza kazi walizopewa kufanya nyumbani.

7. Jitahidi kuwa na kipindi kinachowasaidia wote kujisikia sehemu ya masomo na majadiliano. Usifanye mafundisho kwa haraka.

8. Usiwalazimishe wanafunzi kupokea shabaha za somo. Uwe tayari kusikiliza maoni na mahitaji yao.

9. Usiseme sana bali uwape wote, yaani kila mmoja, nafasi ya kusema na kuuliza maswali.

10. Unapofundisha jitahidi kutega masikio yao. Kumbuka: 1) tumia maneno yanayoeleweka, 2) tumia lugha inayofaa, 3)sema kwa kundi nzima, 4) badili sauti mara kwa mara, 5) kazia kila wazo jipya, 6) punguza idadi ya mambo ya kukazia, 7) usitumie muda mrefu kuwachosha, na 8) wachekeshe mara kwa mara.

11. Buni mbinu tofauti za kufanya katika masomo. Usibanwe na ratiba tu.

12. Onyesha bidii na moyo wako.

13. Omba uongozi wa Roho Mtakatifu wakati unapoandaa na kuongoza masomo.

# MWONGOZO WA KUFUNDISHA VIONGOZI WATUMISHI

## Utangulizi

Mwongozo huu unao mpango wa kukusaidia wewe kuwa na mafundisho kwa viongozi wa kanisa lako katika kujifunza *Kielelezo cha Kibiblia kwa Mafunzo ya Viongozi wa Kanisa.* Mpango huu unaweza kufaa kwa kundi kubwa na hata dogo. Masomo matano yamepangwa kama yafuatavyo hapa chini:

Somo 1: Mtazamo wa Kibiblia juu ya Uongozi, Sehemu wa Kwanza (Utangulizi, Sura ya Kwanza, Sura ya Pili)

Somo 2: Mtazamo wa Kibiblia juu ya Uongozi, Sehemu wa Pili (Sura ya Pili)

Somo 3: Karama za Kiongozi Mtumishi (Sura ya Tatu)

Somo 4: Kumtayarisha Kiongozi Mtumishi (Sura ya Nne)

Somo 5: Hatua Saba za Kuwafunza Viongozi (Sura za Tano na Sita)

## Shabaha za Kujifunza

Shabaha kwa jumla ni kusaidia washiriki:

1. Wapate kuelewa zaidi mitazamo ya Kibiblia juu ya uongozi.
2. Watambue karama zao za kiroho.
3. Wajitoe kabisa kuwa sehemu ya huduma za Kristo katika kanisa lao na jamii.

## Hatua za Kufuata Kupanga Mafundisho

1. Tangaza somo siku ya Ibada. Tangaza kusudi lake na kisa cha fundisho hilo pamoja na siku na saa za kuanza. Hakikisha washiriki wote wamesikia tangazo. Baada ya kozi unaweza ku chagua hasa wale watakaoendelea na mafunzo kufuatana na uongozi katika Sura 4.

2. Agiza vitabu *Kielelezo cha Kibiblia kwa Mafunzo ya Viongozi wa Kanisa* mapema. Hakikisha unazo nakala za kutosha. Waandikishe watakaosoma na wapatie nakala zao kabla hujaanza masomo kwanza. Waulize kusoma Sura 1 na 2.

3. Tengeneza kadi na orodhesha masomo yaliyotajwa katika Utangu lizi. Tumia kadi hii wakati wa masomo.



"diakonos" au "mtumishi". Neno la pili linalotumiwa katika mstari wa 44 ni "doulos" au "mtumwa".

Kitenzi (verb) kinachochimbuka kutoka kwenye neno "diakonos" kina maana ya "kupakua chakula mezani", "kugawa au kutunza", "kuhudumia", au "kutumikia". Neno hilo lilikuja kuwa na maana ya upendo unaofanya kazi, upendo wa Kikristo kwa ajili ya jirani yako. Neno hili halina maana ya yule anayetawala bali yule anayetumikia.

Neno "doulos" au "mtumwa" lina maana ya "aliyefungwa kwa" au "anayetawaliwa na". Kwa vyovyote vile neno hili lililipuka kama baruti masikioni mwa wafuasi wa Yesu siku ile walipokuwa wakitembea kwenye barabara ya mavumbi wakielekea Yerusalemu. Hakuna jambo lililokuwa la kuchukiza zaidi na lisilopendwa na Wayahudi wa karne ya kwanza kama wazo la utumwa.

Katika dunia ya karne ya kwanza, utumwa ulikuwa umeenea sana katika dola yote ya Kirumi. Vita, uharamia, uzao wa kitumwa na madeni vilisababisha kukua kwa utumwa huu mbaya. Mwanahistoria mmoja alisema kwamba idadi ya watumwa ililingana na idadi ya watu huru katika Dola ya Kirumi. Mtumwa alifikiriwa kuwa wa kiwango cha chini cha binadamu kuliko watu huru.

Kwa sheria mtumwa alihesabiwa pamoja na mali na bidhaa hakuwa na haki na asingelimiliki mali. Hata mke wake na watoto hawakuwa wake. Familia zingaliweza kutengwa kama bwana alivyotaka.

Neno "mtumwa" lilikuwa neno mojawapo la matusi mabaya sana ambalo mtu angaliweza kumtukana mwenzake. Kama mtu angalimwita jirani yake mtumwa, basi chuki ya kudumu, uchungu, na ushindani kwa vyovyote vile vingalitokea.

Kwa kuwa watumwa walidharauliwa hivyo, lilikuwa jambo la kawaida kwamba watu walikataa na kudharau aina yoyote ya huduma ambayo ilionyesha dalili ndogo sana ya kufanana na kazi ya mtumwa. Hata hivyo, Yesu alitumia maneno "mtumishi" na "mtumwa" kueleza aina ya hali ya juu sana ya uongozi!

## Yesu ni Kielelezo Chetu

Lakini kabla Yesu hajafundisha juu ya utumishi, alionyesha kwa mfano maana ya kuwa mtumishi wa kweli. Aliishi kama mtumishi miongoni mwa watu. Yesu alichagua shughuli ya utumishi kama kielelezo kinachoongoza cha maisha yake.

Mojawapo ya maandiko ya Biblia yanayotoa muhtasari wa Kristo ni nani na alifanya nini ni katika Wafilipi 2:5-11. Hiki ni kimojawapo cha vifungu muhimu kuhusu Kristo katika Agano Jipya. Kinaonyesha Yesu akitoka kwenye nafasi ya juu sana, hadi duniani, akifa msalabani halafu akirudi tena kwenye

nafasi ya ukubwa ambayo kwayo kila goti litapigwa. Tunaona kwamba maisha ya Kristo yalipitia milele iliyopita hadi milele ijayo.

Sasa fungua Biblia yako kwenye Wafilipi 2:5-11 na soma kifungu hicho. Unaposoma, andika orodha ya mambo yanayodhihirishwa na kifungu hicho kuhusu Yesu ni nani na alifanya nini.

| Wafilipi 2:5-11 | |
|---|---|
| Yesu ni Nani | Yesu Alifanya Nini |
| | |

Wafilipi 2:5-11 inafundisha asili ya Kimungu ya Kristo, kuwako kwake kabla ya ulimwengu, usawa wake na Mungu Baba, kutwaa mwili wa kibinadamu na utu wake kifo chake msalabani, ushindi wake huo juu ya uovu, na utawala wake mbinguni na duniani.

Kifungu hicho pia kinafundisha wazi wazi kwamba Yesu alikuja duniani kama mtumishi. Kwa utashi wake aliweka kando utukufu wake na haki zake akiwa Mungu ili azaliwe kama mtoto mchanga na aishi kama mwanadamu na afe kama mhalifu. Yesu kwa utashi wake, katika kitendo cha juu sana cha unyenyekevu katika historia nzima ya mwanadamu, aliachilia mbali heshima yake na utukufu. Alijivua Umungu akawa mtumishi alifuata njia yote hadi kwenye kifo chake msalabani.

Maisha ya Yesu na huduma yake akiwa kama mtumishi vinaonekana katika Injili zote. Mapema wakati wa huduma yake, alirudi Nazareti alikokuwa amekulia. Alikwenda kwenye sinagogi siku ya Sabato na alikaribishwa kusema siku hiyo. Marafiki zake na majirani walikuwa wamesikia mambo ya



## Mambo ya Kuwazia

1. Tumia dakika chache ukifikiria uongozi wako na wajibu wako katika sehemu ya kuwafunza watakaokuwa viongozi.

- Kuna tofauti gani za kisasa kati ya wachungaji na waumini? Je, hizi ni tofauti za Kibiblia?
- Je,washiriki wa kanisa langu hujifikiria wahudumu (watumishi)kanisani na wa jumuiya? Kwa nini au kwa nini hawajifikirii hivyo?
- Ni hatua gani zichukuliwe kurudisha dhana yaAgano Jipya ya huduma ya waumini?
- Nini maana ya "kuwakamilisha watakatifu hata kazi ya huduma itendeke"? (Waefeso 4:12)
- Nawezajekuwasaidia watu wangu waelewe kwambakila Mkristo ni mhudumu?
- Kwa nini ni muhimu mchungaji kuwa kielelezo katika sehemu ya uongozi wa kitumishi?
- Kwa nini ni vigumu kuwa kielelezo?
- Nahitajiwa kuutumia namna gani muda wangu ninapotaka kuwa kielelezo?
- Nitende nini ili niwe kielelezo bora?
- Nawezajekutumiamasomoyasurahiikatika kuwafundisha na kuwafunza watu wangu?

2. Tumia dakika chache ukihakiki na kufikiria masomo yote ya kitabu hiki. Utachukua hatua gani maalum kuwafunza na kuwatayarisha kikamilifu viongozi watumishi kanisani mwako? Tumia nafasi iliyopo nyuma kuandika mpango wa hatua utakazochukua.

2. Ni kwa njia zipi mtu huyu ameonekana kama kielelezo kwako? Ziandike hapa chini.

_______________

_______________

_______________

_______________

_______________

3.Kwa vipi mafunzo wakati wa kazi yanatumia dhana ya kielelezo kuwafunza watakaokuwa viongozi?

_______________

_______________

_______________

## Muhtasari

1. Kila Mkristo ni mhudumu.
2. Kila Mkristo awe ametayarishwa kikamilifu kwa ajili ya huduma.
3. Kazi muhimu ya mchungaji ni kuwakamilisha waumini.
4. Mchungaji lazima alitumie jicho maalum jambo la kuwafunza na kuwastawisha viongozi watumishi.
5. Uongozi wa kitumishi "unaambukizwa" kuliko"kufundishwa".
6. Mchungaji ndiye kielelezo.



kustaajabisha aliyokuwa akiyatenda. Walikuwa na shauku ya kumsikiliza mtoto wa mji wa nyumbani kwao aliyekuwa ametenda mema.

Yesu alisimama kusoma. Watu wote walikuwa wamemkazia macho. Alichukua kitabu cha Isaya na kuanza kusoma.

Soma Luka 4:18-30 katika Biblia yako uone kilichotokea. Rejea kwenye mistari 18-19 na orodhesha mambo matano ambayo Yesu alikuja kutenda.

1. _______________
2. _______________
3. _______________
4. _______________
5. _______________

Katika mahubiri haya ya ufunguzi Yesu alisema wazi kwamba maisha yake yatakuwa ya utumishi. Alikuja kuwahubiri maskini habari njema, kuwatibu waliovunjika moyo, kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, kuwapa uoni vipofu, na kuwasaidia walioteswa na waliovunjika. Alikuja kubeba mzigo wa maumivu na mahitaji ya wanadamu, wala siyo kuwatawala. Alikuja, siyo kutumikiwa, bali kutumikia.

Habari hii katika Nazareti ilitumika kama ajenda ya huduma ya Yesu. Alitumia muda wake katika utumishi wa wengine. Alimfikia mkoma, alikuwa na wakati kwa ajili ya mtu aliyepooza mwili, alimtibu mwamamke aliyekuwa mgonjwa kwa muda wa miaka kumi na miwili. Kwa furaha alihudhuria karamu ya waliokataliwa na wenye dhambi, aliwakaribisha wale waliokuwa wamelemewa na mizigo mizito waende kwake awapumzishe. Yesu alimfikia kila mmoja aliyekutana naye, awe ni mtu wa tabaka la juu la mahakama ya Kiyahudi aliyemjia usiku, au mwanamke aliyechoka ambaye maisha yake yalitiwa doa na ndoa tano zilizovunjika, au mtoza ushuru asiye na utu aliyetaka kumwona Yesu kuliko kitu chochote, au mwanamke mwenye woga aliyekamatwa na Mafarisayo wakati akifanya uzinzi, au yule aliyesemekana ni rafiki ambaye alimsaliti kwa vipande thelathini vya fedha, ambavyo vilikuwa, kwa mzaha, ni bei ya utumwa.

1. Je, huduma ya Yesu inavyoelezwa katika Luka 4:18-19 inaonyesha nini kuhusu kazi ya kiongozi mtumishi?

_______________

_______________

_______________

2. Utaona katika Luka 4:28-29 ya kwamba Yesu alikutana na upinzani kutoka kwa watu wa mji wa nyumbani kwao. Je ukweli huu unaonyesha nini kuhusu kupendwa na kukubalika kwa kiongozi-mtumishi wakati mwingine?

________________________________________

________________________________________

________________________________________

Yesu alikuwa mtumishi. Ukweli huu unajidhihirisha hapa na pale kwenye kurasa za Agano Jipya. Yesu alijitaja kama "Mwana wa Adamu", ambaye hakuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi (Mathayo 20:28). Maisha yake yalikuwa na tabia ya utumishi. Alijitoa kabisa kwa ajili ya wengine.

Yesu alipothibitisha wajibu wake kama mtumishi, alikuwa anafuata mtindo uliokuwa umeonyeshwa miaka mamia mengi, mapema zaidi katika Agano la Kale. Watumishi wawili wa mwanzoni wanadhihirika katika Agano la Kale. Mmoja ni taifa la Israeli, na mwingine ni Masihi aliyeahidiwa. Manabii wa Agano la Kale walitaja Mkombozi ajaye atakayekuwa mtumishi wa Bwana.

Isaya 42:1-7 inaeleza Mkombozi ajaye. Soma kifungu hicho katika Biblia yako na yatambue mambo matatu: (1) uhusiano wa mtumishi huyu kwa Mungu, (2)mwelekeo wake wa kimawazo na anavyoiendea huduma yake, na (3) huduma yake.

Sasa kamilisha chati ifuatayo. Rejea kwenye kifungu cha Biblia wakati ukikamilisha chati hiyo.

Mtumishi Katika Isaya 42:1-7

| Uhusiano Wake kwa Mungu |
| --- |
| |



5. Jambo gani lifanywe kukuwezesha kuhudumu kwa ufanisi zaidi kama mkamilishaji? Andika mawazo yako au mapendekezo hapa chini.

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

## Umuhimu wa Mchungaji kama Kielelezo

Uongozi wa kitumishi "unaambukizwa" kuliko unavyoweza "kufundishwa". Maisha ya mchungaji na huduma vivae utumishi na kuuonyesha utumishi wa kweli. Tabia zako, mwelekeo wa mawazo yako, mtindo wa maisha, na matendo ya mchungaji ni vya muhimu sana katika kuwafunza viongozi. Lazima uvae na uonyesha kwa mfano maishani mwako mwelekeo wa mawazo, mikazo yenye maana, na dhana ambazo utafundisha.

Mwito wa Yesu kwa wanafunzi wake ulikuwa "Nifuate". Utaratibu wake wa kufuata katika ustawi wa kiongozi haukuwa wa kielimu bali wa uhusiano. Lengo lake lilikuwa kubwa zaidi kuliko utoaji wa ujuzi. Lengo lake lilikuwa ni mawasiliano ya kufanana. Yesu alikuwa kielelezo kamili.

Paulo aliweza kuliandikia kanisa la Korintho, "Basi, nawasihi mnifuate mimi",(1 Kor.4:16); "Mnifuate mimi kama mimi nanavyomfuata Kristo",(1 Kor.11:1). Alimkumbusha Timotheo juu ya uhusiana wao mkubwa na kaa yao pamoja. "Bali wewe umeyafuata mafundisho yangu, na mwenendo wangu, na makusudi yangu, na imani, na uvumilivu, na upendo, na saburi, tena na adha zangu na mateso".(2 Tim. 3:10-11).

Ili wale watakaokuwa viongozi waweze kukuona kama kielelezo, pawepo na hali ya umoja. Mwalimu na mwanafunzi wanapaswa wawe pamoja kwa uhusiano na kwa kushirikiana. Ukweli wa vitendo uwe ni uzoefu kwa wote pamoja katika hali ya kukubaliana, uelewano, na upendo. Yesu aliwaambia wanafunzi, "Nimewachagua muwe pamoja nami".(Marko 3:14). Alianzisha uhusiano wa kuaminiana, urafiki, na upendo kati yake na wale kumi na mmoja.

1. Wafikirie watu katika maisha yako ambao wamepata kuwa vielelezo. Andika jina la mtu ambaye alikuvutia sana maishani mwako.

________________________________________

Timotheo. Alimkumbusha Timotheo wajibu wake kama mkamilishaji na wajibu wake ya kuwakamilisha wengine. "Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine." (2Timotheo 2:2)

1. Tumia dakika chache ukitafakari juu ya huduma yako kama mchungaji. Unatumiaje muda wako? Orodhesha shughuli muhimu au kazi unazozifanya kama mchungaji.

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

2. Karibu ni asilimia ngapi ya huduma yako inayojihusisha na kukamilisha na kuwafunza wengine kwa ajili ya huduma yao? Andika asilimia hapa

_______________________________________________

3. Umewafunza viongozi wangapi? Je, umetumia muda wako wa kutosha na huduma katika kuwafunza angalao watu wawili kwa ajili ya uongozi wa kitumishi? Andika majina ya viongozi wawili uliowakamilisha.

_______________________________________________

_______________________________________________

4. Ni matatizo yapi makubwa au vizuizi vinavyokuzuia usitumie sehemu kubwa ya muda wako kuwakamilisha wengine wapate kuhudumu? Viorodheshe vizuizi hapa chini.

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________



| Mwelekeo Wake wa Mawazo na Anavyoiendesha Kazi |
| --- |
| |

| Huduma Yake |
| --- |
| |

Kifungu hiki kinafundisha kwamba Masihi ajaye atakuwa mtumishi wa Mungu. Atakuwa anampendeza Mungu na atajazwa na Roho wa Mungu. Mwelekeo wake wa mawazo na mwenendo kikazi utakuwa wa mtumishi wa kweli. Atakuwa mkimya na mpole kuliko kuwa mwenye kupaza sauti na mwenye manung'uniko. Atawahurumia wenye mahitaji na kuwafikiria. Hataweza kukatishwa tamaa bali atabakia mwenye matumaini na hodari.

Huduma ya Masihi itakuwa ile ya mtumishi wa kweli. Atawaletea mataifa yote haki na mwanga. Atawawezesha vipofu waone na atawaweka huru wafungwa.

Sura ya Isaya 53 inaeleza kinaganaga kwa uchungu gharama ya utumishi katika huduma ya Masihi. Soma mistari 1-9 ya sura hii na orodhesha mateso aliyovumilia na sadaka iliyofanywa na Kristo.

| Gharama ya Juu ya Utumishi katika Isaya 53:1-9 | |
|---|---|
| Mateso Aliyovumilia Kristo | Sadaka Aliyofanya Kristo |
| | |

Siyo tu kwamba Yesu alichagua utumishi kama msingi na mtindo wa uongozi wake, bali pia aliwaambia wafuasi wake wafuate mfano wake. Alifundisha mengi kuhusu uongozi wa kitumishi. Alisema waziwazi, "Mwenye kuiona nafsi yake ataipoteza, naye mwenye kuipoteza nafsi yake kwa ajili yangu ataiona".(Mathayo 10:39) Yesu alifundisha kwamba mtu akiyahurumia maisha yake kwa uchoyo, mtu huyo kwa kweli atayapoteza, ni kwa kuyapoteza maisha yake katika huduma ya sadaka kwa ajili ya watu wengine ndipo mtu kwa kweli atayapata maisha katika maana iliyo kamilifu kabisa.

Kifungu cha Luka 22:24-27 ni fundisho kuu la Yesu kuhusu utumishi. Tumia dakika chache ukikisoma kifungu hicho. Jiulize mwenyewe,"Kifungu hiki kinafundisha nini kuhusu utumishi?"

Andika kwa muhtasari, ukitumia maneno yako, unayofikiria ni fundisho lipi muhimu la kifungu hicho kuhusu utumishi. Halafu fikiria njia ambayo kwa hiyo unaweza kutumia fundisho hili kuu katika maisha yako.

Fundisho Kuu la kifungu hiki kuhusu utumishi:

________________________________________

________________________________________

Jinsi ninavyoweza kutumia fundisho hili katika maisha yangu:

________________________________________

________________________________________



Kila Mkristo ni mhudumu. Wito wa kuhudumu huenda pamoja na wito wa kuokoka. Wajibu wa huduma hauwezi kupewa mtu mwingine. Kila Mkristo anawajibika kwa Mungu kwa ajili ya huduma yake.

Pamoja na ukweli kwamba kila Mkristo ni mhudumu, ni ukweli ulio sawa na huo kwamba kila mwamini anapaswa kuimarishwa na kufunzwa tayari kwa huduma yake.

Neno linalotumiwa "kukamilisha" katika Waefeso 4:12 ni neno "katartismon", kutoka lugha ya Kiyunani. William Barclay, mtaalumu wa kuchambua maana ya maneno ya Kiyunani, anaonyesha kwamba neno hili linatumiwa kuunganisha kiungo kilichovunjika, au kuweka mahali pake kiungo kilichoteguka. Linatumiwa kuleta amani kwa mji uliobomolewa kwa vita au mapigano, linatumiwa kueleza kustawisha sehemu za mwili kwa njia ya mazoezi, na linatumiwa kueleza kuwa suluhisha marafiki walioachana. "Wazo la msingi la neno ni lile la kuweka kitu au mtu katika hali ambayo mtu au kitu kinapaswa kuwamo."

Neno hili la Kiyunani linatumiwa karibu mara kumi na tatu katika Agano Jipya. Linatumiwa kwa wanafunzi wa Yesu "wakizi tengeneza nyavu zao"(Mt.4:21; Marko 1:19). Yesu alitumia neno hilo katika kumweleza mwanafunzi "ambaye amehitimu" hulingana na mwalimu wake (Luka 6:40). Neno linatumiwa katika Wagalatia 6:1 kwa "kumrejeza upya" au "kumrekebisha" ndugu aliyetenda kosa. Neno hili linatumiwa kuwa na maana ya "kukamilisha" kile ambacho kinapungua".(Tazama 2Kor.13:11; 1Th.3:10; Ebr.13:21; 1 Pet.5:10)

Nani mwenye wajibu wa kuwakamilisha na kuwafunza Wakristo kwa ajili ya huduma yao? Waefeso 4:11-12 inaeleza kwa mkazo kwamba mchungaji ana kazi ya kuwakamilisha watu wa Mungu kwa ajili ya huduma. Kuliko kutenda kazi ya huduma badala ya waumini, mchungaji anahitajika kuwakamilisha watu ili watoke na kuhudumu. Kazi mojawapo ya mchungaji iliyo ya msingi ni kuwa mkamilishaji. Ingawa mchungaji anapaswa kujihusisha na kuwakamilisha waumini wote katika kanisa, hatua maalum ichukuliwe kuwafunza na kuwastawisha viongozi watumishi. Tukijifunza huduma ya Yesu, tutagundua kwamba muda wake mwingi ulitimiwa kuwatayarisha wanafunzi wake wapate kutenda wajibu wao wa uongozi. Aliishi zaidi ya miaka mitatu akiwafundisha wanafunzi wake kumi na wawili. Walitembea pamoja naye, walikula naye, walimsikia akifundisha, walimwona akitenda miujiza, na kuyachunguza maisha yake kinaganaga.

Paulo alitumia sehemu kubwa ya maisha yake katika kuwakamilisha viongozi kwa ajili ya huduma zao. Waraka wake kwa Tito ulikuwa wa kumsaidia mfanyakazi mwenzake aliye mchanga na aliyekuwa msaidizi wake katika huduma yake. Paulo alitumia muda mwingi akifanya kazi na kijana

## SURA YA 6

# UONGOZI WA UCHUNGAJI NA WAJIBU

## Maelezo kwa Jumla.

Wito wako kama mchungaji ni mwito wa huduma ya kukamilisha. Sura hii inashughulikia wajibu wako kama mchungaji katika kuwafunza viongozi. Msingi wa Kibiblia wa huduma yako kama mkamilishaji unachunguzwa na mkazo unawekwa kwenye umuhimu wa mchungaji kama kielelezo.

## Wajibu wa Mchungaji kama Mkamilishaji

Katika Agano la Kale ukuhani ulikuwa wa kikundi maalum cha watu kutoka katika kabila moja maalum. Makuhani walishikilia ya cheo, mbele ya Mungu na walimwakilisha Mungu kwa watu na walimwendea Mungu kwa niaba ya watu.

Mfumo wa Ukuhani wa Agano la Kale ulivunjiliwa mbali wakati Yesu alipokufa msalabani. Alipokuwa anakufa, pazia kubwa Hekaluni lililotenga patakatifu pa patakatifu lilipasuka katikati. (Luka 23:45). Hii ilionyesha kwamba sasa kila mtu aliweza kumwendea Mungu moja kwa moja bila kupitia mtu wa kati (mpatanishi).

Agano Jipya linafundisha mafundisho ya Ukuhani wa waumini wote. Simoni Petro aliwambia Wakristo wote aliposema, "Bali ninyi ni mzao mteule, Ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake, yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu" (1 Petro 2:9).

Sehemu mojawapo ya mafundisho ya Ukuhani wa waumini wote ni kwamba ni wajibu wa kila Mkristo kuhudumu. Waefeso 4:11-12 hufundisha kwamba kila mwamini ana huduma ya kutenda. Soma kifungu hiki kutoka tafsiri mbalimbali. Tafsiri nyingine zinatenga "watakatifu" na "kazi ya huduma". Kituo hiki kilichowekwa mahali kisipostahili kimewaongoza watu wengine kuamini kwamba mchungaji ana kazi tatu za huduma: kuwakamilisha watakatifu, kufanya kazi ya huduma, na kuwajenga waumini wa kanisa. Hii si tafsiri iliyo sahihi.Mchungaji hawezi kufanya kazi ya huduma badala ya waumini. Si wajibu wake kufanya kazi zote; mahubiri, kufundisha, kuwatembelea wagonjwa, kuwahudumia waliofiwa, kuwatembelea washiriki wazembe wa kanisa, na kuwavuta kwa Yesu watu ambao hawajaokoka. Haiwezekani kwa mtu mmoja kufanya kazi hizi zote na hata kama angeweza, kitendo chake kingepunguzia wengine nafasi zao za utumishi na huduma.



Soma vifungu vifuatavyo katika Biblia yako. Andika kwa muhtasari, ukitumia maneno yako, unayofikiria ni fundisho lipi kuu la kila kifungu kuhusu uongozi wa kitumishi.

1. Marko 9:33-37 Fundisho Kuu kuhusu uongozi wa kitumishi:

______________________________

______________________________

2. Luka 14:7-14 Fundisho Kuu kuhusu uongozi wa kitumishi:

______________________________

______________________________

3. Luka 18:9-14 Fundisho Kuu kuhusu uongozi wa kitumishi:

______________________________

______________________________

4. Marko 10:35-45 Fundisho Kuu kuhusu uongozi wa kitumishi:

______________________________

______________________________

5. Mathayo 16:24-28 Fundisho Kuu kuhusu uongozi wa kitumishi:

______________________________

______________________________

6. Mathayo 10:37-39 Fundisho Kuu kuhusu uongozi wa kitumishi:

______________________________

______________________________

7. Yohana 12:20-26 Fundisho Kuu kuhusu uongozi wa kitumishi:

______________________________

______________________________

8. Yohana 10:20-26 Fundisho Kuu kuhusu uongozi wa kitumishi:

______________________________

______________________________

Mojawapo ya mafundisho makuu ya Yesu kuhusu uongozi wa kitumishi ulidhihirishwa vizuri usiku ule kabla hajaenda msalabani. Yesu na wanafunzi wake walikuwa wamekusanyika katika nyumba moja huko Yerusalemu kwa

ajili ya chakula. Desturi ya wakati ule ilikuwa kwamba mtu fulani atawadhe miguu ya watu walipoingia nyumbani. Hali ya ukavu na ya joto pamoja na barabara chafu viliweka tabaka la uchafu kwenye miguu ya kandambili ya wasafiri. Kilikuwa ni kitendo cha kuheshimu kuhakikisha kwamba miguu ya wasafiri kama hao ilitawadhwa. Hata hivyo, kitendo cha kutawadha miguu kilitendwa na mtumwa. Kutawadha miguu kilikuwa kitendo cha utumishi wa kitumwa.

Ni wazi hakuna mtumwa aliyekuwepo wakati huo ili kuosha miguu ya Yesu na marafiki zake. Hakuna mwanafunzi wa Yesu aliyejitolea kufanya kazi hiyo. Inadhihirika kwamba wanafunzi wake walikuwa wamekwisha kubishana ni nani kati yao atakayekuwa mkubwa (Luka 22:24) na walikuwa wamekasirikiana. Waliingia nyumbani na kukaa kimya kwa huzuni. Hapakuwapo kuosha miguu yao!

Chakula kilipakuliwa. Labda wanafunzi wake walikuwa wakingojea waone ni nani atakayeanza. Ni nani atakayepiga hatua mbele, aondoe vazi lake na ajifunge kiunoni na taulo yake? Ni nani atakayekuwa wa kwanza kujaza beseni maji na apige magoti na atawadhe miguu ishirini na minne yenye mavumbi na aipanguse na taulo?

Ghafula wanafunzi wakapigwa na bumbuazi kubwa. Yesu alisimama na kuondoa nguo yake ya nje kabisa. akaenda kando ya chumba. Kila jicho lilikuwa likimwangalia. Kimya Yesu alichukua taulo na kuifunga kiunoni. Kisha akamimina maji ndani ya beseni ya kunawia. Hakuna aliyesema neno. Hewa ya usiku huo ilikuwa ya wasiwasi. Kisha Yesu akapiga magoti karibu na mwanafunzi wa kwanza na akamtawadha miguu na akipangusa na taulo.

Yesu alipopiga magoti karibu na Simoni Petro, mvuvi mwenye ghasia, aliyegeuka kuwa mwanafunzi nakuweza kujizuia zaidi. Akasema kwa dhati, "Haitawezekana wakati wowote unioshe miguu!" Yesu akamwambia Petro ya kwamba kama alitaka kuwa mwanafunzi wake basi amruhusu amtawadhe miguu yake. Mara Petro akabadili mawazo yake na kumtaka Yesu amtawadhe kichwa chake na mikono yake pia.

Baada ya Yesu kuwatawadha miguu yao, alitwaa vazi lake na kuketi kwenye nafasi yake mezani. "Je mmeelewa na hayo niliyowatendea?" akawauliza. "Ninyi mwaniita Mwalimu na Bwana; nanyi mwanena vema, maana ndivyo nilivyo. Basi ikiwa mimi, niliye Bwana na Mwalimu, nimewatawadha miguu, imewapasa vivyo kutawadhana miguu ninyi kwa ninyi. Kwa kuwa nimewapa kielelezo; ili kama mimi nilivyowatendea, nanyi mtende vivyo." (Yohana 13:12-15)

Usiku huo Yesu alifundisha somo kubwa sana kuhusu uongozi duniani. Alionyesha kwa mfano kwamba kazi ya Kiongozi wa kweli ni huduma kwa



wakati wakihudumu. Pia, unaweza kuwa macho kuhusu mahitaji ya mafunzo ya juu na unaweza kuwasaidia watakaokuwa viongozi wajitayarishie mafunzo hayo.

## Muhtasari

Kuna hatua saba za mafunzo ya kiongozi zinazofaa.

1. Gundua mahitaji.
2. Chagua mambo muhimu yanayopasa kuanza.
3. Chagua masomo na taratibu za kufuata. Kuna taratibu tatu za kufuata zinazopaswa kuingizwa katika mafunzo:
   a) Mafunzo ya jumla
   b) Mafunzo maalum
   c) Mafunzo wakati ukifanya kazi
4. Orodhesha wanafunzi watakaokuwa viongozi.
5. Endesha mafunzo.
6. Watambue watu unaowafunza.
7. Fuatilia.

## Mambo ya Kuwazia

Tumia dakika chache ukifikiria jinsi unavyoweza kutumia mpango unaoonyeshwa katika sura hii katika kuwafunza watakaokuwa viongozi.

- Je, nakubaliana na hatua saba za kimsingi katika kuwafunza viongozi watumishi? Je, kuna hatua ambazo naweza kuacha?

- Je, kuna hatua zaidi ambazo naweza kuongeza?

- Je, naweza kubadili mpangilio wa hatua kwa njia yo yote?

- Je, nakubaliana na masomo yaliyoorodheshwa chini ya "mafunzo ya jumla"? Je, kuna sehemu za masomo ambazo naweza kuongeza? Je, naweza kubadili mpangilio wa hatua kwa njia ye yote?

- Je, nakubaliana na masomo yaliyoorodheshwa chini ya "mafunzo maalum"? Je, nitafanya mabadiliko gani?

- Je, nina uzoefu gani katika kuwapangia mafunzoni wale kuwaorodhesha mafunzoni watakaokuwa viongozi? Nitafanya mabadiliko katika ratiba ya mafunzo iliopendekezwa katika sehemu ya 5 "kuendesha mafunzo"?

Kwa kufuata ratiba ya hapo juu, mafunzo ya jumla yatachukua miezi kumi na mitatu. Chati hii inaonyesha jini unavyoweza kupanga mafunzo yako na uhusiano wao ukifuata ratiba hii.

Mafunzo ya Jumla yatadumu kwa muda wa miezi kumi na mitatu.

Mafunzo wakati wa kazi yataanza baada ya miezi sita ya mafunzo ya jumla na yataendelea mpaka wale watakaokuwa viongozi wamekuwa tayari kuchukua nafasi za madaraka.

Mafunzo maalum yataanza pamoja na mafunzo wakati wa kazi na yataendelea mpaka wale watakaokuwa viongozi wamekuwa tayari kuchukua nafasi za madaraka.

Ratiba iliyotajwa imetolewa kuonyesha jinsi mafunzo ya kiongozi yanavyoweza kuundwa na kupangwa. Muda uliopangwa haukusudiwi kuto badilika.

## Watambue Watu Waliofunzwa.

Utambuzi wa watu waliofunzwa ni jambo muhimu sana. Utambuzi wa hadhara kuhusu maendeleo katika mafunzo na huduma utampa kiongozi wa baadaye moyo mkuu wa kujiona ni wa maana na utajenga moyo wa kujiamini na upendo wa kuendelea kujifunza na kukua. Utambuzi pia utahimiza watu wengine wapate mafunzo ya uongozi wa kitumishi.

Utambuzi wa watu waliopata mafunzo unaweza kuonyeshwa kwa njia mbalimbali. Njia mojawapo iliyo nzuri sana ni kufanya ibada inayoshirikisha familia yote ya kanisa. Aina nyingine za utambuzi zaweza kuwa karama ya shukrani, maandishi ya shukrani baada ya wakati fulani katika gazeti la kanisa au gazeti nyingine, chati ya hadhara ukutani inayoonyesha ni nani anashughulikia huduma fulani, barua binafsi kutoka kwako, na "ahsante sana" ya kawaida na inayostahili kutoka kwako na familia ya kanisa.

## Fuatilia.

Ni muhimu kuhifadhi uhusiano wa kirafiki na watakaokuwa viongozi ambao wamemaliza mafunzo yao pamoja nawe. Utaweza kuwasaidia kutafuta nafasi ya madaraka. Kuwatia moyo kwako kutawachochea na kuwaimarisha



niaba ya wengine. Taulo na beseni la kunawia vitadumu kuwa alama kubwa za uongozi wa Kikristo.

Soma Biblia yako katika Yohana 13:1-17 kuhusu Yesu akiitawadha miguu ya wanafunzi wake. Wakati unaposoma, jaribu kufikiria wanafunzi wake walikuwa wanawaza nini Yesu alipokuwa akitawadha miguu yao.

Sasa fikiria majibu ya maswali yafuatayo:

1. Wanafunzi walikuwa wameishi na Yesu kwa muda wa miaka mitatu. Walikuwa wamesikia mara nyingi akifundisha kuhusu utumishi. Unadhani kwa nini hakuna mwanafunzi aliyejitolea kutawadha miguu ya wengine?

2. Kama Yesu angalikuwa hapa sasa katika hali ya mwili, unafikiri angalionyeshaje mfano wa utumishi?

## Mafundisho Mengine ya Kibiblia kuhusu Utumishi

Mtazamo wa kitumishi wa uongozi ulivyotumiwa na kufundishwa na Yesu ilifuatwa na Paulo. Alijitaja kama mtumwa wa Kristo (Warumi 1:1). Wazo la Paulo kuhusu uongozi linaonekana katika 1 Wathesalonike 2:1-12. Alikuwa ameanzisha kanisa katika mji wa kipagani wa Thesalonike. Akilazimishwa kuondoka, aliliandikia kanisa changa barua, muda mfupi baada ya kuondoka, kusaidia kuimarisha imani ya waumini wapya. Aliwakumbusha katika sura ya pili ya waraka wake aina ya maisha aliyoishi alipokuwa pamoja nao.

Soma 1 Wathesalonike 2 na tafuta vidokezi vinavyoonyesha Paulo alikuwa kiongozi wa namna gani. Kufuatana kifungu hiki, mweleze kwa kifupi Paulo kama kiongozi.

Paulo alifundisha katika 1 Wathesalonike 2 kwamba uongozi wa kitumishi unahusiana na mtu kuwa mfano mwema. Alionyesha kwamba makusudi yake yalikuwa safi (ms.3). Shabaha yake ya kuongoza katika maisha ilikuwa ya kumpendeza Mungu katika mambo yote aliyoyafanya (ms.4). Hakuwa amefanya safari ya ubinafsi ili kuwapata watu wa kumsifu (ms.6). Paulo alikuwa tayari kutoa sadaka kwa ajili ya wengine (ms.8). Maisha yake yalikuwa kitabu wazi mbele ya watu na mwenendo wake ulikuwa mbali na lawama (ms.10).

Paulo alieleza malezi aliyoyatoa kwa waumini wachanga katika Uyunani. Anasema juu ya kuwa mpole kama mama anayetunza watoto wake (ms.7). Alifanya kazi miongoni mwa watu akiwa mwenye huruma na baba mwenye upendo miongoni mwa watoto wake; alitia moyo; aliwafariji; na aliwahimiza wampendeze Mungu kwa maisha yao (ms.12).

Simoni Petro alikuwa mtumwa wa Kristo (2 Petro 1:1). Aliandika waraka wake wa kwanza kuwahimiza Wakristo waliotawanyika waishi kama watu waliokuwa wa Kristo, katika 1 Petro 5 alieleza mwenendo wa kufuata ulio sahihi kuhusu uongozi. Ingawa mistari minne ya kwanza ilikuwa imelengwa hasa kwa wachungaji, kifungu chote kina mhusu kila mmoja atakayekuwa kiongozi mtumishi.

Soma 1 Petro 5:1-7. Wakati ukisoma kifungu hicho, kumbuka usiku ule katika chumba cha gorofa wakati Petro alipokuwa hataki Yesu amtawadhe miguu yake.

1. Unafikiri Petro alijifunza nini kuhusu unyenyekevu tangu uzoefu wake katika chumba cha gorofa? (ms.5-6)

________________________________________

________________________________________

2. Unafikiri Petro alijifunza nini kuhusu utumishi tangu usiku ule katika chumba cha gorofa?

________________________________________

________________________________________

3. Kusudi letu liwe lipi tunapofanya kazi yetu, kwa kumfuata Petro? (ms.2)

________________________________________

________________________________________

4. Petro anafundisha nini kuhusu mtu kuwa mfano? (ms.3)

________________________________________



| SEHEMU YA MASOMO | MUDA WA MAFUNZO |
|---|---|
| *Mafunzo ya Jumla* | |
| Mtazamo wa Kibiblia juu ya uongozi | Wiki 4 |
| Karama za Kiroho | Wiki 12 |
| Sifa za viongozi watumishi | Wiki 3 |
| Uanafunzi kwa Wanafunzi wa kimsingi | Wiki 12 |
| (Baada ya miezi sita ya mafunzo ya jumla kila shemasi wa baadaye atapangwa chini ya shemasi aliyekomaa ili achunguzwe na apate mafunzo kazini. Wale watakaokuwa waalimu wa Masomo ya Biblia wa watu wazima watawekwa chini ya mwalimu mwenye uzoefu wapate kujifunza na kufanya kazi naye.) | |
| Ukaguzi ya Biblia | Wiki 12 |
| Ukaguzi ya Mafundisho ya Biblia | Wiki 6 |
| Kujifunza juu ya Kanisa na Kazi Yake | Wiki 3 |
| Ustadi wa Uongozi kwa Ujumla | Wiki 4 |
| *Mafunzo Maalum* | |
| Ustawishaji wa karama maalumu za kiroho (hii inafanywa kama sehemu ya mafunzo wakati wa kazi) | Inaendelea |
| Mafunzo ya Rika (wale watakaokuwa waalimu wa Masomo ya Biblia wa watu wazima wakazanie rika la watu wazima; watakaokuwa mashemasi wapate mafunzo ya jumla ya marika yote) | Wiki 4 |
| Mafunzo Maalum ya huduma (haya yanaweza kwenda pamoja na kutatua matatizo yakitegemea mafunzo wakati wa kazi) | Inaendelea |
| *Mafunzo Wakati wa Kufanya Kazi* | |
| Anza wakati wa mafunzo ya Jumla, mafunzo wakati wa kazi yaendelee mpaka viongozi wa baadaye wawe tayari kuchukua nafasi za madaraka. | Inaendelea |

(Unamwona kwamba ni mwaminifu, yu tayari na anafundishika.) Mweleze mafunzo yatahusu nini (jumla, maalum, mafunzo kazini).

Omba sana kabla ya kuchagua watakaokuwa viongozi kwa ajili ya masomo. Yesu aliomba usiku wote kabla ya kuwachagua mitume wake kumi na wawili.(Luka 6:12-13) Mwombe mtu anayehusika aombee jambo hilo kabla ya kukubali kuingia kwenye mafunzo ya kiongozi wa baadaye.

Rudia tena orodha yako ya watakaokuwa viongozi katika sura hii. Tumia dakika chache ukifikiria namna utakavyoorodhesha kila mmoja mafunzoni kwa njia iliyo bora kabisa.

## Endesha Mafunzo.

Kuliko kuanza kukadiria kwamba mafunzo yako ya kiongozi mmoja au zaidi yatahitaji miezi sita au miezi tisa au mwaka mmoja, itakuwa vizuri kuanza mafunzo na kuendelea nayo mpaka mtu au watu wamepata mafunzo ya kutosha kwa ajili ya huduma. Endapo miezi tisa yaweza kuwa muda wa kutosha kwa kiongozi mmoja, miaka miwili yaweza kuhitajiwa kwa ajili ya mtu mwingine. Mahitaji ya watu binafsi hutofautiana na unahitajiwa kutoweka muda maalum ili uweze kutosheleza mahitaji tofauti.

Masomo ya kila juma yanapendekezwa kwa ajili ya mafunzo. Masomo haya yanaweza kuwa ya kikundi kidogo cha watakaokuwa viongozi au ya mtu mmoja tu. Hapa tena mahitaji na hali za mazingira zitatofautiana na uwe tayari kurekebisha muda vilivyo. Inapendekezwa kwamba uzoefu wa kupatikana kazini uanze mapema wakati wa mafunzo. Siyo lazima kungojea mpaka mafunzo ya jumla na maalum yamekamilishwa kabla ya kuanza mafunzo wakati wa kazi.

Nidhamu kwa upande wako kama mwalimu na kwa upande wa wale watakaokuwa viongozi itahitajiwa wakati wa mafunzo. Mara ratiba ikisha kupangwa, lazima ifuatwe. Utaratibu ovyo wa kupanga na kupangua hautafanikiwa. Umuhimu wa kwanza utolewe kwa vipindi vya mafunzo na visifutwe bila ya sababu za maana sana.

Hebu dhania kwamba unafundisha viongozi watumishi wanne wa baadaye. Wawili wanajifunza kuwa mashemasi na wawili wanajifunza kuhudumia kama waalimu wa Biblia wa watu wazima. Hapa inapendekezwa ratiba ya mafunzo.



Viongozi wa kweli wote wakubwa katika Biblia yote walikuwa watumishi. Walihudumia mahitaji ya watu na kuongoza kwa kutumikia.

Musa aliitwa mtumishi wa Mungu (Kum.34:5). Alijitoa katika huduma ya sadaka kwa ajili ya wengine.

Yoshua alikuwa mtumishi (Yos.24:29). Siyo tu kwamba alikuwa msaidizi wa Musa, alitumia muda wake kuwahudumia wengine.

Manabii kama Eliya (2 Fal.9:36), Isaya (Isa.20:3), Yeremia (Yer.7:25), Amosi (Amo.3:7), Yona (2 Fal.14:25), na Danieli (Dan.6:20) walikuwa watumishi wa Mungu. Shadraka, Meshaki, na Abednego wakiwa vijana waliitwa watumishi wa Mungu (Dan.3:26).


Abrahamu alikuwa mtumishi (Zab.105:42) na Kalebu (Hes. 14:24) na Ayubu (Ayu.1:8). Wafalme kama Daudi (2 Sam.3:18) na Hezekia (2 Nya.32:16) waliitwa watumishi wa Mungu.

Katika Agano Jipya, Yakobo alijiita "mtumwa wa Mungu na wa Bwana Yesu Kristo" (Yak.1:1). Mtume Yohana aliitwa mtumwa wa Kristo (Ufu.1:1) na wengine akina Yuda (Yuda 1), Fibi (Warumi 16:1) na Epafra (Kol.4:12) walikuwa watumishi.

Watumishi wa Mungu katika Biblia walikuwa watu wakubwa. Walikuwa wakubwa kwa sababu walikuwa watumishi. Ukubwa wao ulitegemea utumishi. Maisha yao yalitawaliwa na unyenyekevu, utii na kujikana. Hawakujitakia njia yao; wajitakia njia ya Mungu.



DAUDI



YOSHUA

Tunapojizoeza uongozi wa kitumishi, tunatembea kando kando na kundi kubwa la wanaume na wanawake ambao walijitolea kabisa kwa Mungu. Ni heshima kutumikia.

Biblia iko wazi, kuwa kiongozi wa kweli, mtu anahitaji kuwa mtumishi. Biblia inachofundisha kuhusu uongozi ni kigeni kutokana na mawazo ya kidunia. Lakini ndiyo njia ya kuipata furaha na ukubwa mbele ya macho ya Mungu.

- Njia ya kuwa mkubwa ni kuwa mtumishi.
- Njia ya juu ni chini.
- Njia ya mbele ni nyuma.
- Njia ya kuheshimiwa ni kunyenyekea.
- Njia ya kupanda ni kuzama.
- Njia ya kupokea ni kutoa.
- Njia ya kushinda ni kujitolea.
- Njia ya kupata ni kupoteza.
- Njia ya kufurahi ni kulia.
- Njia ya kupanda ni kutelemka.
- Njia njia ya kuishi ni kufa.

Na mtu mkubwa . . . . . .

- Si yule anayeamrisha, bali anayetii,
- Si yule aliye na watumishi wengi, bali yule anayewatumikia wengi,
- Si yule anayemiliki vingi, bali yule anayetoa vingi.

## Muhtasari

1. Dunia isiyomjua Mungu ina mawazo yaliyo na taabu kuhusu uongozi. Kwa dunia, uongozi unahusishwa na cheo, uwezo, mamlaka, na heshima.

2. Ufunguo kwa uongozi ni Utumishi. Kuwatumikia wengine ni aina ya juu sana ya uongozi.

3. Yesu, kiongozi mkubwa kuliko wote wakati wote, alikuwa mtumishi. Aliishi maisha ya upendo wa sadaka na kujitoa kwa ajili ya wengine.



### 3. Mafunzo Wakati wa Kazi

Utaratibu wa tatu wa kufuata katika kuwafunza viongozi ni mafunzo wakati wa kazi au kujifunza wakati mtu akitenda kazi. Hakuna kinachoweza kuchukua nafasi ya uzoefu katika kujifunza dhana na stadi za uongozi wa kitumishi. Mtu hujifunza kwa kutenda. Mafunzo maalum na ya jumla hayatoshi mpaka yaoanishwe na kujihusisha yenyewe katika huduma. Yesu alitenda mengi zaidi kuliko tu kuwafundisha wanafunzi wake kuhusu huduma. Walijifunza wakati akihudumia na wenyewe wakaenda kuhudumia wakati wa kazi inaonekana katika sehemu ya kushuhudia.

Unapofunza atakayekuwa kiongozi kuhusu namna ya kushuhudia, nenda pamoja naye ili apate kukuona unavyoshuhudia watu ambao hawajaokoka. Halafu nenda pamoja na mtu yule apate kushuhudia wakati ukimwangalia. Halafu msaidie katika sehemu ambazo umeona ni dhaifu na jadiliana na mtu huyo kuhusu alivyotenda kazi yake na namna ya kuitenda vizuri zaidi. Mwishowe, mpeleke mtu huyo ashuhudie na mtu mwingine. Kwa njia hiyo utakuwa unaongeza mafunzo ya watu wa kushuhudia.

Tumia dakika chache ukifikiria namna utakavyoendesha mafunzo wakati wa kazi pamoja na watakaokuwa viongozi. Ni viongozi gani waliokomaa katika kanisa lako? Je, wanaweza kukusaidia katika sehemu hii ya mafunzo? Orodhesha majina yao hapa chini, pamoja na huduma zao maalum au sehemu za uongozi.

| MAFUNDISHO WAKATI WA KAZI | |
|---|---|
| **Watu wa kusaidia** | **Huduma maalum au sehemu za uongozi** |
| | |
| | |
| | |

## Orodhesha Wanafunzi Watakaokuwa Viongozi.

Baada ya kupanga mafunzo ya kiongozi kwa kufuata umuhimu wake, na masomo ya kimsingi na taratibu za kufuata, wakati umefika wa kuorodhesha watakaokuwa viongozi(kwa ajili ya mafunzo). Umekwisha kufahamu watakaokuwa viongozi ni akina nani kanisani mwako. Ulikwisha kuwaorodhesha katika sehemu ya "viongozi wa baadaye".

Orodhesha wanafunzi watakakaokuwa viongozi, ukiwaita mmoja mmoja. Mweleze kila mmoja kwa nini umemchagua kuwa kiongozi wa baadaye.

*C.* Mafunzo Maalum ya Huduma

Atakayekuwa kiongozi anapaswa kupata mafunzo maalum katika kazi maalum au huduma atakayofanya. Kwa mfano, mtu anayejifunza kuwa shemasi anapaswa kufundishwa kuhusu wajibu maalum wa shemasi.

Tumia dakika chache ukitafakari sehemu tatu za masomo zilizotajwa hapo juu. Fikiria namna utakavyoendesha mafunzo haya maalum kwa ajili ya wale watakaokuwa viongozi wa kanisani mwako.

Tena, una misaada gani ambayo itakusaidia katika kutayarisha na kuendesha mafunzo haya maalum? Orodhesha misaada hii chini ya kila sehemu ya somo hapa chini.

Ustawi wa Karama Maalum za Kiroho

________________________________

________________________________

________________________________

Masomo ya Rika

________________________________

________________________________

________________________________

Mafunzo Maalum ya Huduma

________________________________

________________________________

________________________________

Ni nani katika kanisa lako anayeweza kukusaidia kuendesha masomo haya maalum? Kuna uwezekano wa Wakristo katika kanisa lako wanaoweza kufundisha sehemu za mafunzo maalum au kuhudumia kama watu wa misaada kukusaidia? Orodhesha majina yao hapa chini na kando ya kila jina onyesha sehemu maalum ambayo mtu huyo anaweza kusaidia.

| MAFUNDISHO MAALUM | |
|---|---|
| Watu wa kutoa Msaada | Sehemu Maalum |
| | |
| | |
| | |
| | |



4. Tunaitwa tuwe watumishi leo. Ni kwa kupoteza maisha yetu katika huduma ya sadaka kwa ajili ya wengine ndipo mtu wa kweli anapoyapata maisha katika maana yake kamilifu kabisa.

5. Taulo na Beseni la kunawia ni alama kubwa za uongozi wa Kikristo.

6. Paulo na Petro walifundisha kwamba uongozi wa kweli ni Utumishi.

7. Katika maandiko yote ya Biblia, viongozi wa kweli wote wa kubwa walikuwa watumishi.

## Mambo ya Kuwazia

Sasa tumia dakika chache ukifikiria namna unavyoweza kuwafundisha watu wako, hasa wale watakokuwa viongozi baadaye kuhusu mtazamo wa Kibiblia juu ya uongozi. Yafikirie maswali yafuatayo. (Siyo lazima uandike majibu).

- Je washiriki wangu wanatambua mafundisho ya Biblia kuhusu Utumishi?
- Je washiriki wana mawazo gani kuhusu kiini cha uongozi?
- Je mawazo gani yasiyo sahihi waliyo nayo?
- Je washiriki wanaelewa kwa kweli kwamba Yesu alikuwa mtumishi na ya kwamba tunapaswa kufuata mfano wake?
- Je washiriki wanatambua kwamba njia ya kupata furaha na ukubwa mbele ya macho ya Mungu ni njia ya huduma ya Kikristo ya kujitoa na kunyenyekea?
- Nawezaje kutumia masomo ya sura hii, katika kuwafundisha washiriki maadili ya Kibiblia juu ya uongozi?

# KARAMA ZA UONGOZI WA KITUMISHI

## Maelezo kwa Jumla

Ili kugundua, kujitayarisha kikamilifu, na kuwahusisha katika huduma viongozi wengi kutoka kanisani mwako, utahitajiwa kuelewa wazi wazi Biblia inafundisha nini kuhusu karama za Kiroho. Pia utahitaji kuwafundisha wale watakaokuwa viongozi wa baadaye namna ya kugundua na kustawisha karama zao za Kiroho. Sura hii inazungumzia sehemu tatu: (1) Kudhihirisha na kuzieleza karama za Kiroho;(2) Kweli nane za Kibiblia kuhusu karama za Kiroho; na (3) Hatua sita za kumsaidia mtu kugundua karama zake za Kiroho.

## Karama za Kiroho ni nini?

Karama ya Kiroho ni uwezo unaotolewa na Roho Mtakatifu kwa huduma ya Kikristo. Tuna vipaji fulani, vipimo vya akili, na uwezo vinavyotuwezesha tutende huduma. Karama hizi hutoka kwa Mungu. Karama za Kiroho zimeorodheshwa katika nyaraka tatu mbali mbali katika Agano Jipya: Warumi 12:6-8; 1 Wakorintho 12:8-10, 28-30; na Waefeso 4:11.

Karama hizi hutofautiana kwa kiasi fulani kutoka orodha katika Biblia ambayo imekamilika na hatujui kama orodha zote zilizounganishwa zimekamilika au hapana. Wataalamu wengi hufikiria kwamba orodha zimekusudiwa kutoa mifano ya karama za Kiroho kuliko kukamilisha orodha yote.

Fungua Biblia yako na soma Warumi 12:6-8; 1 Wakorintho 12: 8-10, 28-30; na Waefeso 4:11. Orodhesha karama katika jedwali hapa chini wakati unaposoma.

Karama za Kiroho

| Warumi 12:3-8 | 1 Wakorintho 12:8-10,28-30 | Waefeso 4:11 |
|---|---|---|
| | | |



Ukaguzi wa Biblia Yote

______________________________

______________________________

______________________________

Ukaguzi wa Mafundisho ya Biblia

______________________________

______________________________

______________________________

Masomo kuhusu Kanisa na Kazi Yake

______________________________

______________________________

______________________________

Ustadi wa Uongozi kwa Ujumla

______________________________

______________________________

______________________________

2. **Mafunzo Maalum**

Utaratibu wa pili wa kufuata katika kuwafunza viongozi ni kutoa mafunzo maalum. Haya ni mafunzo ya juu zaidi kuliko mafunzo ya jumla; nayo yana shabaha ya kuwaelimisha viongozi katika sehemu maalum. Angalau sehemu tatu za masomo lazima ziwe sehemu ya mafunzo haya:

*A.* Ustawi wa Karama Maalum za Kiroho

Baada ya masomo ya kimsingi ya karama za kiroho zinazoelezwa chini ya mafunzo ya jumla, atakaye kuwa kiongozi asaidiwe katika kugundua na kustawisha karama zake za kiroho. Kwa mfano, kama yule atakayekuwa kiongozi akigundua kwamba ana karama ya Uinjilisti, mafunzo maalum lazima yatolewe kumsaidia astawishe karama hiyo.

*B.* Masomo ya Rika

Atakayekuwa kiongozi anapaswa kupata mafunzo maalum kuhusu rika (kikundi chenye umri sawa) ambalo atakuwa akifanya kazi nalo. Tabia za washiriki wa rika fulani, na namna ya kufanya kazi nao, lazima vieleweke katika masomo.

*H.* Ustadi wa Uongozi kwa Ujumla

Ustadi wa uongozi kwa ujumla ni namna ya kufanya kazi na vikundi lazima uwe sehemu ya mafunzo ya jumla kwa ajili ya wale watakaokuwa viongozi.

Tumia dakika chache utafakari sehemu nane za masomo zilizotajwa hapo juu. Fikiria namna utakavyoendesha mafunzo hayo ya jumla kwa ajili ya wale watakaokuwa viongozi wa kanisa lako. Una misaada gani inayoweza kukusaidia katika kuwafundisha watakaokuwa viongozi kanisani mwako? Orodhesha misaada hiyo chini ya kila sehemu ya somo hapa chini. Baadhi ya misaada imekwisha kuorodheshwa kwa ajili yako.

Mtazamo wa Kibiblia Juu ya Uongozi

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

Karama za Kiroho

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

Sifa za Viongozi Watumishi

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

Uanafunzi wa Wanafunzi wa Msingi

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________



Sasa chunguza orodha tatu ulizotayarisha. Hesabu karama zote. Karama iliyorudiwa rudiwa zaidi ya mara moja ihesabu kama ilivyo karama moja. Andika jumla hapa________. Hesabu halisi hutofautiana, kwa kutegemea jinsi baadhi ya karama zinavyo unganishwa. Karama zingine huungana. Hii hufanya kazi ya kutenga karama kutoka kwa nyingine iwe ngumu. Watu wengine huhesabu karama tofauti kumi na nane au kumi na tisa. Tena, watu wengine hufikiri kwamba orodha hii ya karama haikukamilika.

Jambo moja lazima liwe wazi. Kila Mkristo anaamrishwa kutumikia katika shughuli za karama hizi, ikiwa anayo karama fulani au hapana. Kutokuwa na karama fulani katika maisha ya Mkristo haimpi udhuru wa kutotii amri ya Utumishi katika shughuli fulani ya karama. Kwa mfano, tunaamriwa sote kutoa. Ati kwa sababu mwamini hana karama maalumu ya utoaji, haina maana kwamba apuuzie kutoa. Sote tunaamriwa kushuhudia bila kujali kuwepo au kutokuwepo kwa karama ya Uinjilisti. Karama ya Uinjilisti ni kipawa maalumu wanachopewa watu wengi, lakini sote tunategemewa kuungana na wengine katika imani yetu. Sote tunategemewa kuonyesha huruma. Wakristo wengine wana kipawa maalum katika jambo hili.

Hebu tuchunguze karama hizi kwa undani zaidi. Soma chati ifuatayo. (Ile sehemu isiyo na maandiko iache kwa wakati huu.)

| **Chati ya Karama** | | |
|---|---|---|
| **Unabii** (kuhubiri) | Kuhubiri Neno la Mungu kwa uongozi wa Roho Mtakatifu | |
| **Utumishi** (huduma, kusaidia) | Kutenda kazi ya upendo na ya kufaa kwa ajili ya wengine | |
| **Kufundisha** | Kuwasiliana na kueleza Neno la Mungu kwa watu wengine | |
| **Ushauri** (kusauri, kutia moyo) | Kuzungumza mambo ya kufaa kutia moyo na kuimarisha wengine | |
| **Kutoa** (kugawana) | Kuwashirikisha wengine kwa vitu na kazi Bwana kwa uhuru uchangamfu | |
| **Kuongoza** | Kuwasaidia watu kufuata nafasi zinazowafaa na kuwatia moyo na kuwapa msaada unaohitajiwa ili kazi itendeke | |
| **Huruma** | Kuwahurumia na kwa vitendo kuwapa mahitaji wale wenye shida. | |

| | | |
|---|---|---|
| **Hekima** | Uwezo wa kuhusisha kweli za Mungu kwenye mahitaji na matatizo ya maisha. | |
| **Maarifa** | Uwezo wa kuelewa ukweli wa Mungu. | |
| **Imani** | Kuona kile ambacho Mungu anataka kitendeke na kuwa na imani isiyotikisika kwamba Mungu atakitenda. | |
| **Utambuzi** (uono wa kiroho) | Kupambanua kati ya roho ya ukweli na roho ya uwongo. | |
| **Utume** | Maana yake rasmi, karama hii ilikuwa kwa mitume wa kwanza wa Kristo; katika maana yake pana zaidi, hii ni karama ya kuweza kuhudumu kama mmisionari kwa watu wa utamaduni mwingine. | |
| **Uinjilisti** | Kuwasilisha Injili kwa wasioamini watu wapate kumpokea Yesu kama Mkombozi. | |
| **Uchungaji** | Kwenda kuongoza na kuwajenga Wakristo katika kukua kiroho na huduma. | |
| **Uponyaji** | Kuingilia kwa nguvu za Kimungu katika kutibu ugonjwa bila ya matumizi ya njia za kimaunbile. | |
| **Miujiza** | Kusababisha matukio yatokee ambayo hayawezi kuelezeka kwa sheria za kimaumbile. | |
| **Ndimi** (lugha) | Wataalamu hutofautiana kuhusu jambo hili, kuna tafsiri mbili: (1) kusema katika lugha ngeni ambayo hukujifunza kwa njia za kawaida, au (2) kusema misemo bila kufikiri ambayo haiwezi kueleweka. | |
| **Kutafsiri ndimi** | Hapa tena, kuna tafsiri mbili: (1) kutafsiri wakati lugha ya kigeni inapozungumzwa kabla hujajifunza lugha, au (2) kutafsiri misemo isiyo ya kufikiri wakati inapoweza kueleweka.. | |



akajikamua katika sehemu yake ya udhaifu, akajirekebisha na kufikia viwango vinavyohitajiwa.

Rudia Sura ya Nne ukifikiria kutumia masomo na wale watakaokuwa viongozi kanisani mwako.

*D.* Uanafunzi wa Wanafunzi wa Msingi

Watakaokuwa viongozi wanapaswa wafundishwe dhana rahisi za kimsingi katika sehemu za uanafunzi wa wanafunzi (uanafunzi wa Kikristo wa kimsingi) na ukuaji wa Kikristo. Msaada utolewe kuhakikisha kwamba kila atakayekuwa kiongozi ni Mkristo na anayekua. Umuhimu wa saa za kukaa kimya kila siku peke yako pamoja na Mungu, kujifunza Biblia, kuomba, kukariri vifungu vya Biblia, kushiriki pamoja na Wakristo wengine na kuwashuhudia wasio Wakristo vinapaswa vifundishwe.

Kitabu kinachoitwa *Nifuate* ni masomo mazuri sana yanayohusu uanafunzi kwa wanafunzi wa kimsingi na yanayofaa kuyatumia pamoja na watakaokuwa viongozi. Hii ni kozi ya majuma kumi na moja, kozi ambayo atakayekuwa kiongozi anaweza kujisomea mwenyewe na kuimaliza au inaweza kutumiwa kama msingi wa kikundi cha kujifunza. *Nifuate* inapatikana katika lugha ya Kiswahili ama Kiingereza, hata lugha nyingine nyingi. Kuna vitabu vingine vinavyoitwa *MasterLife*. Kozi nzima ni vitabu saba pamoja na kitabu cha uongozi. Vitabu hivi vyote vinapatikana kutoka:

Baptist Publications
S.L.P. 30405
Nairobi, Kenya

Kwanza uliza kwenye duka la vitabu ulipopata kitabu hiki.

*E.* Ukaguzi ya Biblia Yote

Unapaswa uwape watakokua viongozi mafundisho ya Biblia nzima. Unapaswa ushughulikie mada za msingi zilizomo katika Biblia. Utakuwa msaada kuwapa mambo muhimu ya kila kitabu cha Biblia.

*F.* Ukaguzi ya Mafundisho ya Biblia

Watakaokuwa viongozi wanapaswa wafahamu vizuri mafundisho ya kimsingi ya imani yetu ya Kikristo. Mafundisho kuhusu Mungu, Kristo, Roho Mtakatifu, mwanadamu, na wokovu yanapaswa yafundishwe. Vitabu mbalimbali vya kimsingi vinavyohusu mafundisho mbali mbali ya Kikristo vimeorodheshwa katika vitabu vya kumbukumbu.

*G.* Masomo kuhusu Kanisa na Kazi Yake

Mafundisho ya kanisa, kazi au shughuli za kanisa na muundo wa serikali wa kanisa vinapaswa vifundishwe kwa watakaokuwa viongozi wote.

kufuata. Uamue mambo yatakayokuwamo ambayo utashughulikia chini ya kila utaratibu wa kufuata.

1. **Mafunzo ya Jumla**

Mafunzo ya jumla ni mafunzo yanayohusu mambo ya jumla utakayowafundisha wale watakaokuwa viongozi wa baadaye. Haya ni mafunzo ya msingi ambayo kila atakayekuwa kiongozi anahitaji, bila kujali mahitaji yake au sehemu ya huduma anayotegemea kufanya. Angalau sehemu nane za masomo zinapaswa ziwemo katika muhtasari wa mafunzo ya jumla.

*A.* Mtazamo wa Kibiblia Juu ya Uongozi

Kila atakayekuwa kiongozi anapaswa kufundishwa kwamba mtazamo wa Kibiblia juu ya uongozi ni utumishi. Hili ni jambo la msingi na la lazima ukiwa msingi wa kujengea. Atakayekuwa kiongozi asipoelewa kiini cha kweli cha uongozi, mafunzo yake yote yatakuwa hayana msingi na yatakosa lengo.

Sura ya Pili katika kitabu hiki inaeleza masomo ya kutumia katika kufundisha mtazamo wa Kibiblia juu ya uongozi kwa wale watakaokuwa viongozi.

Rudia Sura ya Pili ukiwa na wazo akilini mwako la kutumia mafunzo hayo na wale watakaokuwa viongozi katika kanisa lako. Njia mojawapo ya kutumia masomo ni kuwahusisha watakaokuwa viongozi. Katika mfululizo wa Masomo ya Biblia vitumia vifungu vya Biblia chini ya kila kichwa katika Sura ya Pili. Unaweza kutoa utangulizi wa somo hili kwa kueleza "mtazamo wa dunia kuhusu uongozi". Halafu mkafanya masomo ya Biblia chini ya vichwa vingine vya sura (Utumishi ndio Ufunguo, Yesu ndiye Kielelezo chetu, na mafundisho mengine ya Kibiblia kuhusu utumishi).

*B.* Karama za Kiroho

Uelewaji wa karama za kiroho ni wa msingi kwa uongozi wa kitumishi unaotenda kazi. Sura ya Tatu katika kitabu hiki ina masomo ya kutumia katika kufundisha somo hili kwa wale watakaokuwa viongozi katika kanisa lako. Rudia Sura ya Pili ukifikiria kutumia masomo hayo na wale watakaokuwa viongozi katika kanisa lako.

*C.* Sifa za Viongozi Watumishi

Sura ya Nne inatilia mkazo kwamba vipimo ni vya juu kwa wale wanaohudumu wakiwa viongozi watumishi. Vipimo hivi, viwango, au sifa vinapaswa vifundishwe kwa kila atakayekuwa kiongozi. Ni jambo muhimu kiongozi mtumishi kufahamu sifa za uongozi ni zipi. Hii haina maana kwamba mtu anayepungukiwa na sifa moja au zaidi kwa vyovyote vile aondolewe katika orodha ya watakaokuwa viongozi. Ina maana ya kwamba anaweza



Watu hutofautiana vikubwa kuhusu karama nne za mwisho: uponyaji, miujiza, ndimi, na kutafsiri lugha. Kuna angalao mawazo matatu kuhusu karama hizi za "alama".

1. Wakristo wengi wenye imani huamini kwamba vipawa (karama) hivi maalum vilipewa kanisa la mwanzoni wakati wa uchanga wake ili kuthibitisha kazi ya Mungu katika jamii ya Kipagani na ya kwamba vipawa hivi havionekani tena katika maisha ya kanisa.

2. Wakristo wengine, na enye imani, huamini kwamba vipawa hivi maalum bado hutolewa sasa katika sehemu za dunia ambako Injili inahubiriwa kwa mara ya kwanza na vizuizi vinahitajika kushindwa.

3. Bado na wengine, pia wenye imani, huamini kwamba vipawa hivi vyote ni sehemu muhimu sana ya kanisa la leo.

Bila ya kujali tafsiri ya vipawa hivi maalum, jambo moja ni wazi. Tafsiri ya mtu isiwe kipimo cha kuwa mshiriki. Tunatakiwa tuwakubali na kuwapenda watu wanaoshikilia mawazo tofauti na yasiwe mawazo ya kutenga watu. Kusudi la vipawa vya kiroho ni kujenga, siyo kugawanya.

Yakupasa utambue kwamba karama hizi zote zimetolewa kumwezesha mpokeaji kuwasaidia wengine. Hasa, karama zote ni karama za utumishi. Wakristo wote wanaitwa kuwa viongozi watumishi. Na hata tuwe na karama zipi, zinatakiwa zitumiwe kwa faida ya wengine.

Hebu tusome Biblia na tuone baadhi ya karama za kiroho zinazotumiwa na watu wa Mungu. Soma kila kifungu kilichoorodheshwa hapa chini. Halafu katika safu ya mkono wa kulia andika karama unayoona ikidhihirishwa na mtu katika kifungu. Rejea kwenye chati ya karama uliyotoka kusoma katika sura hii.

| Kifungu cha Biblia | Watu | Karama Inayodhihirika |
|---|---|---|
| 1. Matendo 2:14-41 | Petro | |
| 2. Matendo 9:36 | Dorkasi | |
| 3. Matendo 17:1-4 | Paulo | |
| 4. Matendo 9:26-27 | Barnaba | |
| 5. Matendo 4:32-35 | Wakristo wa Mwanzoni | |
| 6. Kutoka 18:13-27 | Musa | |
| 7. Luka 10:25-37 | Msamaria Mwema | |
| 8. 1 Wafalme 3:16-18 | Sulemani | |
| 9. Matendo 13:1-3 | Barnaba na Sauli | |

Hapa kuna majibu tuliyoyapata tuliposoma vifungu. Majibu yako huenda hayatakubaliana na yetu kwa kila hali. Hiyo ni sawa kwa sababu karama zinaungana; na karama maalum siyo rahisi kuitambulisha. Petro - Unabii; Dorkasi - Huduma; Paulo - Ualimu (kufundisha); Barnaba - Ushauri; Wakristo wa Mwanzoni - Kutoa; Musa - Kuongoza; Msamaria Mwema - Huruma; Sulemani - Hekima; Barnaba na Paulo - Utume.



Tumia dakika chache kurudia tena chati ya karama. Unaposoma kila maelezo, fikiria mtu ambaye kwa mawazo yako, ana karama fulani. Andika jina la mtu yule kwenye safu ya mkono wa kulia. (Zile karama za "alama" hazihesabiwi katika zoezi hili).

## Kweli Nane za Biblia kuhusu Karama za Kiroho

1. **Roho Mtakatifu ni Karama ya Mungu kuliko zote kwa Mwamini.** Mtu anapomwamini Kristo kama Bwana na Mwokozi, Mungu ambaye ni Roho Mtakatifu huja kuishi katika maisha yake. Roho Mtakatifu mwenyewe ni Karama kuu ya Mungu kwa kila mwamini. Kuweko kwa Roho katika maisha yetu ni chemchemi ya uwezo wetu wa kuhudumu.

2. **Kila Mkristo ana angalao karama ya kiroho moja, yawezekana zaidi.** Tuna vipawa. Kuna neno zuri katika Agano Jipya lenye maana ya "enye kipawa". Watu wengine wanachukua neno hili katika ibara yake na kulitumia kuwataja watu wanaonena kwa lugha. Hii ni kosa. Neno hili lina maana ya "enye karama" na linapotumiwa katika maana yake ya Kibiblia



zipi zinazohitajika kustawishwa zaidi katika kanisa langu? Orodhesha karama za kiroho zinazohitaji sana kustawishwa katika kanisa lako.

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

Sasa rudia na jikumbushe masomo yako katika sehemu tano hapo juu. Mahitaji katika sehemu hizi tano yanawakilisha mahitaji ya mafunzo ya kiongozi katika kanisa lako. Umemaliza hatua ya kwanza katika kupanga mafunzo yako ya kiongozi.

## Panga mambo kwa kufuata umuhimu wake.

Haiwezekani kufanya mara moja kila kitu kinachohitaji kutendeka katika sehemu ya mafunzo ya kiongozi. Kwa vyovyote vile umetambua mahitaji mengi zaidi kuliko unavyoweza kuyashughulikia mara moja. Unapaswa kupanga mahitaji ya mafunzo ya kiongozi katika kanisa lako na chagua ni yapi utayashughulikia kwanza. Hii ndiyo maana ya "kuchagua kwa kufuata umuhimu."

Kutokana na mahitaji yote ya kiongozi ambayo umegundua, chagua mahitaji matano yaliyo ya chini kwa mpango wa umuhimu zaidi (anza na hitaji muhimu zaidi kuliko yote).

1. ____________________________________
2. ____________________________________
3. ____________________________________
4. ____________________________________
5. ____________________________________

Kadiri ya mahitaji haya yanavyotekelezwa unaweza kwa taratibu kuanza kupanga kutekeleza mahitaji mengine ya kiongozi katika kanisa lako.

## Chagua Yatakayokuwamo Mafunzoni na Taratibu za Kufuata.

Hatua hii inahusu namna utakavyopanga kukabili mahitaji muhimu ya mafunzo ya kiongozi katika kanisa lako. Unahitajiwa ufikirie taratibu tatu za

3. **Nafasi za Kuimarisha**

"Fundo dhaifu" katika kanisa lako ziko wapi? Ni nafasi zipi ambazo hivi karibuni zimejazwa ambazo zinahitaji kuimarishwa? Kwa mfano, inawezekana kuna waalimu watatu wa Masomo ya Biblia ambao ni waalimu dhaifu na ambao wanahitaji msaada ili waendelezwe. Orodhesha nafasi za uongozi katika kanisa lako ambazo zinahitaji kuimarishwa.

4. **Viongozi wa Baadaye**

Ni akina nani katika kanisa lako ambao wanaweza kuwa viongozi wa baadaye? Ni nani katika kanisa lako ni mwaminifu, yu tayari, na anafundishika? Orodhesha wanaoweza kuwa viongozi.

5. **Karama Zisizotumika**

Ni karama zipi za kiroho zinazoonekana hazitumiki miongoni mwa ushirika wa kanisa lako? Kwa mfano, kama kanisa lako halikumvuta mtu yeyote kwa Kristo mwaka uliopita, basi bila shaka karama ya Uinjilisti inahitaji kustawishwa miongoni mwa washiriki wako. Usielewe vibaya jambo hili. Roho Mtakatifu hugawa karama za kiroho kwa kufuata utashi wake wa kifalme. Sisi hatuchagui au kufanyia kazi karama za kiroho. Hata tunapaswa kushughulikia ustawi wa karama tulizopewa na Roho Mtakatifu.

Rejea kwenye "Chati ya Karama" katika Sura ya Tatu. Soma tena kila karama na maelezo yake. Unapokuwa ukichunguzachati hii, jiulize, "Ni karama



linaweza kutumika kwa sisi wote. Sisi ni "charismatic" (wenye karama) kwa sababu tu watu wa Mungu walio na karama.

3. **Wakristo wote hawana karama za kiroho zilizo sawa.** Sura ya 12 ya 1 Wakorintho inatilia mkazo mgawanyiko tofauti wa karama. Paulo anaulinganisha mwili wa Kristo na mwili wa Kibinadamu na anaonyesha jinsi kila sehemu ya mtu ni ya lazima ili mwili wote upate kufanya kazi kwa umoja. Kila sehemu ya mwili inahitaji sehemu zingine. Unahitajika. Umaarufu. Mtu fulani alisema kwamba ugonjwa wa Kansa unasababishwa na chembe hai moja iliyofikiri haihitajiwi. Unahitajiwa na Mungu. Unahitajiwa na wengine. Kwa kuwa u mtu wa pekee, una sehemu ya pekee inayohitajiwa uijaze. Mojawapo ya mafundisho muhimu katika Agano Jipya ni kwamba mwili wa Kristo, Kanisa, hauwezi kufanya kazi sawasawa mpaka kila mwamini ametimiza wajibu wake wa kipekee. Una kazi maalum ya kufanya, na hakuna mwingine anayeweza kuifanya sawasawa kama wewe unavyoweza. Upekee wetu tu ni karama kutoka kwa Mungu na tunatakiwa kuitumia kwa ukamilifu. Huduma yetu kama viongozi watumishi inakuzwa na jinsi tulivyo na wajibu wa pekee tunaoweza kutenda.

4. **Hakuna mwamini aliye na vipawa vya kiroho vyote.** Tumeumbwa tutegemeana. Kila moja anamhitaji mwenzake. Kuna huduma unayoweza kufanya katika mwili wa Kristo ambaye hakuna mwingine tena katika dunia anayeweza kuifanya sawasawa kama unavyoweza. Bwana Mungu anamhitaji kila mmoja wetu. Mwili wa Yesu haukamiliki mpaka kila mwamini mwanamume au mwanamke anatimiza wajibu wake.

5. **Waongoze washiriki kukubali karama zinazoonekana kupewa na Roho Mtakatifu.** Paulo anadhihirisha jambo hili: "Lakini kazi hizi zote huzitenda Roho huyo mmoja, yeye yule, akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye." (1 Wakorintho 12:11) Hatuamui tutakuwa na karama zipi. Uchaguzi unafanywa na Roho Mtakatifu.

6. **Kusudi la karama ni kuujenga mwili wa Kristo, watu wa Mungu.** "Kila mmoja kwa kadiri alivyoipokea karama, itumieni kwa kuhudumiana; kama mawakili wema wa neema mbali mbali za Mungu." (1 Petro 4:10) Mtazamo wa kitumishi juu ya uongozi unaonekana wazi katika jambo hili. Karama zetu za kiroho zinatuwezesha kuhudumia kama viongozi watumishi.

7. **Kila Mkristo anaamriwa kuwa mwaminifu na mwenye bidii katika kutumia karama zake.** "Basi kwa kuwa tuna karama zilizo mbali mbali, kwa kadiri ya neema tuliyopewa." (Warumi 12:6) Tutajieleza jinsi tunavyotumia karama zetu.

8. **Tusiwaonee wivu na husuda watu walio na karama zinazodhihirika zaidi.** Hapa tena, Paulo anaeleza jambo hili wazi katika 1 Wakorintho 12 kwa kulinganisha mwili wa binadamu. Soma mistari 21-26. Tumia dakika

chache ukifikiria kanisa lako katika mwanga wa kweli hizi nane za Kibiblia. (Majibu yaliyoandikwa si ya lazima.)

- Je Roho Mtakatifu anadhihirika katika maisha ya waumini wengi kanisani mwako?
- Je kuna mwamini anayejihisi hafai aliyeachwa katika mambo yanayohusu karama? Kwa nini Wakristo wengine huhisi kwamba "hakuna ninachoweza kufanya"?
- Je kuna mgawanyiko wa karama za kiroho ulio wazi kanisani mwako? Nani katika kanisa lako ana karama zinazodhihirika kidogo kama huruma, ushauri(kutia moyo), na utoaji?
- Ni kwa njia zipi waumini wa kanisa lako wanategemeana na kuhusiana?
- Je waumini wako wanaelewa kwamba Roho Mtakatifu ndiye anayeteua nani atapata karama ipi?
- Je waumini wako wanaelewa kwamba kusudi la karama ni kulikuza na kulijenga kanisa?
- Je kuna waumini katika kanisa lako ambao si watumishi waaminifu katika matumizi ya karama zao za kiroho?

## Namna ya kuwaongoza washiriki wa kanisa lako kugundua karama zao.

Tumeona kwamba Biblia inamhimiza kila mwamini kuwa mwaminifu katika kutumia karama zake lakini haitoi maelezo au utaratibu namna ya kugundua karama zetu. Paulo hasemi, "Sasa ndugu, hizi ndizo hatua za kufuata katika kugundua karama zako za kiroho."

Sehemu hii imeandikwa kukupa mwongozo na madokezo ya kufuata kuwasaidia washiriki wa kanisa lako kugundua karama zao za kiroho. Kuna maneno mawili ya kufikiria kabla hujaanza kuwafundisha. Kwanza, inakupasa kuwatia moyo wale wanaojaribu kugundua karama zao wasiwe na wasiwasi ikiwa mara hawawezi kuzitambua karama zao. Uwakumbushe kuna Wakristo wengi waaminifu wanaomtumikia Mungu kwa njia nzuri bila ya kuweza kueleza karama zao ni zipi.

Pili, wasaidie wale unaowafundisha wasiweke fikra zao zote kwenye karama ambazo wanafikiri wanazo na kusahau sehemu zingine za madaraka. Kwa mfano, mmoja angeweza kusema, "Sifikiri kwamba nina karama ya



**SURA YA 5**

# HATUA SABA KATIKA MAFUNZO YA KIONGOZI UTUMISHI

## Maelezo kwa Jumla

Kuna msingi wenye sehemu tatu kuhusu mpango au utaratibu wa kufuata katika kuwafunza viongozi wa kanisa la mahali fulani. Msingi huo umeundwa na: (1) Mtazamo wa Kibiblia juu ya uongozi ambayo ni utumishi, (2) Ukweli ya kwamba kila mwamini amepewa karama za kiroho, na (3) Kipimo cha Kibiblia au sifa za uongozi wa kitumishi. Mara mtu akielewa msingi huu wenye sehemu tatu, yu tayari kutengeneza mpango unaofaa kwa ajili ya kuukuza uongozi.

Sura hii inawasilisha mpango unaofaa kutumika kuwafunza vion gozi watumishi. Mpango wa hatua kwa hatua umetolewa, nao unahusu: (1) Kugundua mahitaji ya mafunzo ya uongozi; (2) Kupanga mambo kwa kufuata umuhimu wake; (3) Kuchagua mambo yanayopasa kuwamo katika mafunzo na utaratibu utakaofuatwa; (4) Kuorodhesha watakaokuwa viongozi; (5) Kuendesha mafunzo; (6) Kuwatambua viongozi wanaofunzwa; (7) Kufuatilia wale unaowafunza.

Kuna taratibu za kufuata na mipango kwa mafunzo ya kiongozi. Kila mchungaji anayejihusisha katika mafunzo ya viongozi ana mtindo wake maalum au utaratibu wa kufuata. Hapa kuna hatua saba kwa mafunzo ya kiongozi ambazo zimethibitika zinafaa. Unapojifunza kila hatua, jiulize, "Nawezaje kutekeleza hatua hii katika mafunzo ya kiongozi kanisani mwangu?"

## Gundua Mahitaji.

Hatua ya kwanza katika mafunzo ya kiongozi ni kugundua mahitaji ya mafunzo ya kiongozi ni yapi. Kwa maneneo mengine, unapaswa utafute ni kipi kitendeke kanisani mwako katika sehemu ya mafunzo kiongozi. Mara chache mchungaji hugundua kwamba kuna viongozi wengi waliopata mafunzo, hivyo hakuna mahitaji yoyote. Kila kanisa linahitaji viongozi watumishi zaidi waliopata mafunzo.

Ili kugundua mahitaji, unatakiwa kujikagua, na kwa uangalifu uchunguze na kulitalii kanisa lako. Angalau sehemu tano zinapaswa zichambuliwe.

1. **Malengo ya Kanisa na Mahitaji.**

Chunguzamalengo na mahitaji ya kanisa lako. Malengo hasa ya kanisa lako ni yapi? Mnaelekea wapi? Ujumbe wenu ni upi? Mnatumaini kutekeleza nini kama kanisa? Kila kanisa linapaswa kujihusisha katika kazi au shughuli

Ni katika sehemu gani hapo juu ulipojikadiria ?_____________ Unaweza kueleza kwa nini katika sehemu hizo umekadiria hivyo? Utachukua hatua gani kurekebisha hali hiyo?

## Muhtasari

1. Tuwapime watu kwa akiba ya uwezo wao - kwa hali wanayoweza kuwa nayo baadaye.

2. Watakaokuwa viongozi wa baadaye wanapaswa kuwa waaminifu, waliotayari kutumikia, wanaofundishika.

3. Sifa za Kibiblia kwa kiongozi mtumishi ni za juu lakini mtu anaweza akawa nazo.

4. Moyo wa kitumishi ni wa lazima kwa uongozi wa kitumishi.

5. Uongozi wa kitumishi si kile ambacho mtu anatenda bali ni jinsi mtu alivyo.

6. Maisha ya kiroho ya kiongozi mtumishi ni muhimu sana chemchemi yake ya uwezo ni Roho Mtakatifu, Neno la Mungu, maombi, na ushirika na waumini wengine.

## Mambo ya Kuwazia

Fikiri unavyoweza kutumia masomo ya sura hii katika kuwafunza viongozi watumishi katika kanisa lako.

- Ni akina nani wanaoweza kuwa viongozi wa baadaye katika kanisa langu ambao wanajitokeza mara moja akilini mwangu?

- Nawezaje kutumia sifa za viongozi watumishi katika 1Timotheo 3 na Tito 1 katika kuwafunza viongozi watumishi kanisani mwangu?

- Nawezaje kutumia "tao la uongozi wa kitumishi" katika kutoa mafunzo kwa viongozi watumishi kanisani mwangu?

- Nawezaje kuwachochea na kuwahimiza viongozi wa baadaye wawe na nidhamu ili wapate kufikia sifa na viwango vya uongozi wa kitumishi?



uinjilisti, kwa hivyo siwezi kuwashuhudia watu wengine." Hii ni kosa ambalo wanapaswa waliangalie wasilitende.

Kweli mbili muhimu zinapaswa zitiliwe mkazo kabla ya kusoma mwongozo unaohusu namna ya kugundua karama. Ukweli wa kwanza ni kwamba mtu awe ni Mkristo ili aweze kupokea karama za kiroho. Uwezo huu maalum kwa ajili ya kuhudumu hupewa washiriki wa mwili wa Kristo peke yao.

Ukweli wa pili ni kwamba kila mwamini amepewa karama moja ya kiroho au zaidi. Hili limekwisha kuzungumzwa. Tunapaswa kutambua kwamba tuna karama.

Sasa kuhusu mwongozo. Hapa kuna mapendekezo sita kukusaidia katika kuwaongoza washiriki wa kanisa lako kugundua karama zao za kiroho. Mapendekezo haya ni mwongozo tu wa kufuata wakati mtu akiomba na kutafuta karama zake ni zipi.

1. **Waongoze washiriki kujitoa kabisa kwa Mungu na kumtegemea Roho Mtakatifu ili awaongoze.** Panga hotuba za Jumapili, mafundisho au majadiliano maalum kuwaongoza washiriki kujitoa kabisa kwa Bwana Kristo kila siku katika kila sehemu ya maisha yao. Waongoze kumwomba Mungu awasaidie kugundua karama alizowekesha amana kwao.

2. **Waelekeze washiriki kujifunza Biblia kwa utaritibu.** Kujifunza Biblia kwa mpango wa kila siku ni lazima kwa Mkristo ili apate kukua. Ni kwa kujifunza Biblia ndipo tunajua karama za kiroho ni zipi. Ungeanza madarasa ya masomo ya Biblia kwa rika zote. Pia, ungetafuta njia za kuwasaidia washiriki wote kuwa na mpango wa kusoma Biblia na kuomba nyumbani mwao. Hii ni lazima kwa kukua kwa Mkristo. Kupitia masomo ya Biblia, tunajifunza juu ya karama za Roho. Ni kwa kusoma kitabu cha Matendo na vifungu vingine ndipo tunapoona karama za kiroho zikitumiwa na waumini katika mwili wa Kristo. Ujuzi kuhusu Biblia inafundisha nini juu ya karama za kiroho unatusaidia kutambua karama walizo nazo Wakristo wengine. Kwa kuyaona maisha yao, pia huimarisha na kupanua kuelewa kwetu karama zenyewe.

3. **Washughulishe washiriki katika utumishi wa kanisa.** Usiwaruhusu kukaa na kungojea mpaka ati wamefahamu karama zao za kiroho kabla hawajajishughulisha na utumishi. Kwa kweli kujihusisha katika huduma ni jambo muhimu katika kugundua karama zao. Shughuli za mahitaji ya kanisa lako na jumuiya ni zipi? Utaweza kutenda nini kuwasaidia kutimiza mahitaji hayo? Fanya jaribio. Washughulishe katika huduma mbalimbali katika kanisa lako. Wape kazi mbalimbali za kujitolea. Kufanya hivi siyo tu kwamba kunawasaidia wapate mwanga bora kuhusu shughuli za karama mbalimbali; bali kunawasaidia waelewe vizuri zaidi. Watagundua kile wanachoweza kukifanya vizuri na kile ambacho hawafanyi vizuri.

4. **Tambua mielekeo yao.** Omba ili upate kugundua karama zao. Orodhesha mawazo yako juu ya mielekeo na mapendeleo yao. Kisha zungumza na kila mmoja juu ya mawazo yako. Unaweza kukaza mawazo yao au kuwapa mawazo mapya. Waulize maswali kama haya: Mielekeo yako ni ipi? Unapenda kufanya lipi? Ni sehemu zipi za huduma unazopenda? Unahisi hali ya moyo wa kuamini au kupendelea aina fulani za huduma? Je una mzigo wa huduma fulani?

Waelekeze washirki kujipima kwa uaminifu na uwezo wao, mambo yakoje? Wasaidie kupima shughuli wanazofanya na majibu ya wale wanaowahudumia. Usijiweke juu, bali utia moyo kwao. Ikiwa wanakosa, uwaongoze kuzijaribu karama zingine katika sehemu zingine za huduma. Fanya uamuzi unaostahili ulivyo. (Warumi 12:3)

5. **Waongoze washiriki wa kanisa kuuliza na kupata uthibitisho kutoka kwa waumini wengine.** Kanisa hutenda wajibu muhimu katika kumsaidia mtu agundue karama zake. Waumini wengine mara nyingi huona dalili za karama za kiroho katika maisha ya mtu. Familia ya kanisa yenye upendo na yenye kuhimiza mtu ni ya muhimu sana katika kusaidia mtu kutafuta sehemu ya huduma. Jambo lenye maana sana ni kwa wewe kuwa kielelezo. Wewe mwenyewe unaweza kuwauliza wengine mawazo yao kuhusu karama zako. Tena, tumia masomo mbalimbali kufundisha washiriki kutambua na kuhimiza karama zao.

Wakati mwingine Wakristo wengine hutambua kwamba mtu fulani anayo karama ya kiroho kabla ya mtu huyo hajaigundua karama yake. Mnamo miaka ya mwanzoni ya karne ya 19 washiriki wachache katika kanisa dogo la Texas walitambua karama ya uchungaji aliyokuwa nayo kijana mwanamume aliyejitoa na ambaye alijishughulisha kwa uaminifu kanisani. Kijana yule alikuwa hajafikiria kuwa mchungaji. Viongozi wa kanisa walimwendea kijana yule na wakamsadikisha imani yao.Kijana yule alikubaliana na uamuzi wa kanisa na akaanza kuhubiri na kuwa mchungaji. Mtu yule, anayejulikana katika dunia kama Dr. George W. Truett, aligeuka kuwa mmojawapo wa viongozi watumishi wakubwa wa karne hiyo.

6. **Wasaidie washiriki wakubali karama ambazo zionekana Mungu amewapa na zitumie kwa unyenyekevu kwa ajili ya Yesu.** Tumia njia tofauti katika kanisa kuwasaidia washiriki kuwashukuru kwa vile wanavyoweza kufanya katika mwili wa Kristo na vitende kwa moyo wa upendo. Katika ibada zenu wape washirki nafasi ya kujitoa karama zao kwa utumishi wa Kristo na kuzitumia karama zao zote jinsi wawezavyo. Tafuta kustawisha karama zao na zitumie kikamilifu kabisa. Shairi hili ni kweli:

"Uhai mmoja tu, mara utatoweka,

kitendwacho kwa ajili ya Kristo tu ndicho kitadumu."



kutawaliwa na Roho. Kiongozi mtumishi wa kweli ni mtu anayetawaliwa na Roho Mtakatifu.

Asili ya pili ya uwezo ni Biblia. Hakuna kinachoweza kushika nafasi ya Neno la Mungu katika maisha ya kiongozi mtumishi. Kusoma Biblia kila siku na kulitafakari Neno la Mungu hutoa nguvu ya kuhudumia wengine.

Asili ya tatu ya uwezo ni maombi. Mungu anazungumza nasi kwa njia ya Biblia na sisi tunazungumza naye kwa maombi. Yote mawili ni muhimu. Ni jambo la lazima kwa kila kiongozi mtumishi kuwa na wakati wa kimya kila siku na kuudumisha kwa ajili ya kujifunza Biblia na kuomba.

Asili ya nne ya uwezo ni ushirika. Ushirika na waumini wengine wa umri mbalimbali ni asili ya uwezo kwa kiongozi mtumishi. Maisha ya Kikristo hayakukusudiwa kuwa maisha ya upweke. Hakuna kilicho bora zaidi kama familia ya kanisa yenye uchangamfu, upendo na kujali.

Kamilisha zoezi lifuatalo la kujitambua. Jipime kwenye mizani ya kila usemi kama unavyofikiria. Chora mviringo kwa namba inayohusika na jibu lako.

| | Mara Chache | Mara kwa Mara | Kila Mara |
|---|---|---|---|
| 1. Ninatambua kuwako kwa Mungu katika maisha yangu kila siku. | 1 | 2 | 3 |
| 2. Natazamia kila siku kusoma na kujifunza Biblia | 1 | 2 | 3 |
| 3. Nasoma Biblia kila siku. | 1 | 2 | 3 |
| 4. Biblia huzungumza nami ninapoisoma. | 1 | 2 | 3 |
| 5. Maombi ni sehemu muhimu ya maisha yangu. | 1 | 2 | 3 |
| 6. Ninaomba uongozi wa Mungu katika mambo madogo kama nifanyavyo katika mambo makubwa. | 1 | 2 | 3 |
| 7. Ninahudhuria ibada za kuabudu za kanisa langu kila juma. | 1 | 2 | 3 |
| 8. Ninatazamia kuwa pamoja na familia ya kanisa langu kila juma. | 1 | 2 | 3 |
| 9. Roho Mtakatifu anaishi hasa katika maisha yangu. | 1 | 2 | 3 |
| 10. Maisha yangu yanatawaliwa na Roho Mtakatifu. | 1 | 2 | 3 |

Vifungu zaidi vya Biblia vinavyohusu uongozi wa Kitumishi vimeorodheshwa hapa chini. Soma kila kifungu na tafakari kifungu hicho kinasema nini kuhusu uongozi wa Kitumishi. (Haihitajiwi kuandika majibu, labda ukitaka.)

| | |
|---|---|
| 1 Wathesalonike 5:15 | Yakobo 5:16 |
| 1 Timotheo 4:12 | 1 Petro 1:22 |
| Tito 2:7 | 1 Petro 2:17 |
| Waebrania 3:13 | 1 Petro 4:9 |
| Waebrania 13:2 | 1 Yohana 3:11 |
| Yakobo 4:11 | 1 Yohana 3:16-18 |

Orodhesha hapa chini majina ya watu wawili ambao unawaona kila siku.

1. ____________________

2. ____________________

Fikiria njia mbili ambazo kwazo unaweza kuwahudumia zaidi watu hawa.

1. ____________________

2. ____________________

## Maisha ya Kiroho ya Kiongozi Mtumishi

Uongozi wa kitumishi si kile ambacho mtu anatenda, bali zaidi ni jinsi *alivyo*. Tabia ni muhimu zaidi kwa uongozi wa kitumishi kuliko *shughuli*. Uongozi wa kitumishi ni tabia, thamani na mwelekeo wa mwamini aliyejitoa kwa matendo yanayoonyesha kufanana na Kristo katika hali yake alivyo na kutenda.

Mtindo wa maisha wa kiongozi mtumishi unapingana na njia ya maisha ya dunia. Mtu anahitaji zaidi ya nguvu za kimwili kukamilisha mahitaji ya uongozi wa kitumishi. Nguvu za Kimungu zinahitajiwa ili mtu aishi maisha ya kitumishi.

Yesu anagawa nguvu hiyo. "Naweza kuikabili kila hali kwani Kristo hunipa nguvu". (Wafilipi 4:13) Kwa kweli Kristo *ndiye* uwezo. Kupitia kwa Roho Mtakatifu, Kristo anaishi katika kila mwamini kwa kuongoza, kufundisha, kufariji, kuimarisha, na kutoa uwezo. Kujazwa na Roho Mtakatifu ina maana ya



Kazi ya kugundua karama zetu inaweza kuchukua muda mrefu. Mara nyingi hatuzigundui kwa haraka kama tutakavyo. Tusikose tumaini na kukata tamaa kabisa. Tunahitajika kubakia waaminifu kazini kama watumishi wema wa Yesu Kristo.

Zamani kulikuwa kundi la wafanyakazi waliopewa kazi ya kuchukua mizigo kwenye sehemu za milima. Akisafiri usiku, kila mfanya kazi alichukua mzigo mkubwa kwenye mabega yake. Taa ndogo iliyofungwa kwenye kila goti ilitoa mwanga hafifu wa kumwezesha kuona njia nyembamba. Taa zilikuwa ndogo.Hazikuweza kutoa mwanga kwa njia iliyopindapinda ili kumwezesha mpagazi kuona mbali sana. Aliweza tu kuona futi chache mbele yake. Lakini ilimradi mtu aliendelea kutembea, mwanga ulitosha. Mwanga uliendelea kwa kila hatua aliyopiga. Kama mpagazi alisimama, hata mwanga ulizimika. Alihitajika kuendelea kutembea. Ilimradi aliendelea kufanya hivyo, alikuwa na mwanga wote aliouhitaji.

Kadiri tunavyojitoa kuwa viongozi watumishi na kujitoa kuwahudumia wengine, Mungu atatuimarisha kikamilifu kutupa mwanga wa kutosha tunaohitaji ili tuweze kumtendea kazi.



Tumia dakika chache ufikirie karama zako za rohoni.

1. Orodhesha karama zinazoonekana zaidi katika maisha yako na huduma.

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

2. Kwa kifupi eleza ulivyoweza kutambua karama zako za kiroho.

______________________________

______________________________

______________________________

## Muhtasari

1. Karama ya kiroho ni uwezo unaotolewa na Roho Mtakatifu kwa ajili ya utumishi wa Kikristo.
2. Kuna angalau karama za kiroho kumi na nane, labda nyingi zaidi.
3. Karama zote za kiroho ni karama za utumishi.
4. Karama iliyo kubwa kuliko zote aliyo nayo mwamini ni Roho Mtakatifu.
5. Kila Mkristo ana karama moja ya kiroho au zaidi.
6. Wakristo wote hawana karama za kiroho zilizo sawa.
7. Hakuna mwamini aliye na karama zote.
8. Roho Mtakatifu huamua ni nani atapata karama ipi.
9. Kusudi la karama ni kutusaidia tuwe viongozi watumishi na kuujenga mwili wa Kristo.
10. Tunawajibika kwa namna tunavyotumia karama zetu. Hivyo tuwe waaminifu.
11 :imwonee wivu mtu aliye na karama iliyo tofauti na yetu.
12. Tunapaswa kutafuta ni karama zipi za kiroho ambazo tumepewa.Hata hivyo, tusikate tamaa au kufa moyo tusipoweza kugundua karama zetu mara moja.
13. Hakuna hatua zilizoorodheshwa katika Biblia jinsi mtu anavyoweza



Kamilisha jedwali ifuatayo:

| Sehemu ya Marekebisho | Hatua Nitakazochukua |
|---|---|
| 1. ______ | ______ |
| 2. ______ | ______ |

## Uongozi wa Kitumishi katika Matendo

Katika tao la mawe, jiwe lililo juu kabisa linalofanana na nyenzo huitwa "jiwe la ufunguo". Jiwe hili limewekwa mahali pa ulinzi kabisa kwa vile hushikilia tao lote pamoja. Angalia katika kielelezo ukurasa wa 42 kwamba jiwe la ufungu ni *Moyo wa Utumishi* (Wafilipi 2:5). Tabia hii ni ya lazima kabisa kwa uongozi. Kama sifa zingine zote zipo, lakini sifa hii inakosekana, basi uongozi wa kweli utakuwa haupo. Kumbuka, uongozi ni utumishi!

Kamilisha mafunzo ya Biblia hapa chini na utaona tunavyohimizwa tena na tena kuwa na "moyo wa utumishi" na kujizoeza uongozi wa kitumishi. Soma kila kifungu cha Biblia halafu andika maelezo kwa muhtasari ukionyesha kifungu kinavyosema ichukuliwe hatua gani. Vifungu viwili vya kwanza vinakamilishwa kukuonyesha mfano.

**Uongozi wa Kitumishi katika Matendo**

| Kifungu | Hatua Tunazopaswa Kuchukua |
|---|---|
| Warumi 12:10 | |
| Warumi 12:13 | |
| Warumi 14:13 | |
| Warumi 15:17 | |
| 1 Wakorintho 16:14 | |
| Wagalatia 5:13 | |
| Wagalatia 6:2 | |
| Waefeso 4:2 | |
| Waefeso 4:32 | |
| Wafilipi 4:5 | |
| Wakolosai 3:9 | |
| Wakolosai 3:12 | |
| Wakolosai 3:13 | |
| 1 Thesalonike 3:12 | |
| 1 Thesalonike 4:18 | |
| 1 Thesalonike 5:11 | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 13. *Kutawaliwa na Roho Mtakatifu* - ninanyenyekea chini ya uongozi na maelekezo ya Roho Mtakatifu maishani mwangu. | 1 | 2 | 3 |
| 14. *Usafi wa rohoni* - ni safi katika mawazo yangu na vitendo maishani. | 1 | 2 | 3 |
| 15. *Kusudi wazi maishani* - ni naomwelekeo wazi maishani mwangu; nataka maisha yangu yatumiwe katika utumishi kwa ajili ya Kristo, bila kujali kazi nitakayofanya. | 1 | 2 | 3 |
| 16. *Unyenyekevu* - sina kiburi na majivuno; sishikilii mambo yangu tu pekee yake. | 1 | 2 | 3 |
| 17. *Upendo kwa wengine* - ninao upendo halisi kwa watu wengine. | 1 | 2 | 3 |
| 18. *Urafiki* - ni mtu wazi na mwenye kujali na kuwaendea watu wengine. | 1 | 2 | 3 |
| 19. *Shauku ya bidii na kufaulu* - ninayo shauku na moyo unaoamini kwamba nitafaulu. | 1 | 2 | 3 |
| 20. *Uelewano wa mawazo au hali ya wenzangu* ninajali sana na kujihusisha na wenzangu na kushughulikia mahitaji yao. | 1 | 2 | 3 |
| 21. *Siasa ya kuchukuliana na watu* - nina akili ya utu na sisemi maneno yasiyo na busara. | 1 | 2 | 3 |
| 22. *Ucheshi* - nina tabia nzuri ya kutabasamu. | 1 | 2 | 3 |

Chagua tabia mbili kutoka kwenye orodha hapo juu zinazowakilisha sehemu ya maisha yako ambayo marekebisho makubwa yanahitajika. Fikiria hatua maalum unazoweza kuchukua ili kujirekebisha katika tabia hizo mbili.Kwa mfano, kama unataka marekebisho katika *siasa ya kuchukuliana na watu,* unaweza kufikiria hatua kama hizi:

- Uwe mtu wa kupima, wakati wote na kuwajali wengine.
- Usiwe mwepesi sana wa kusema.



kugundua karama za kiroho. Hapa kuna mwongozo:

a. Waongoze washiriki kujitoa kabisa na kuamini Roho Mtakatifu ili awaongoze.
b. Waelekeze washiriki kujifunze Biblia kwa utaratibu.
c. Washughulishe washiriki katika utumishi wa kanisa.
d. Tambua mielekeo yao.
e. Waongoze washiriki wapate uthibitisho kutoka waumini wengine.
f. Wasaidie washiriki wakubali karama ambazo zinaonekana Mungu amewapa na zitumie kwa unyenyekevu kwa ajili ya Yesu.

## Mambo ya Kuwazia

Tumia dakika chache ukifikiria jinsi utakavyowafundisha waumini wako kuhusu karama za kiroho. Fikiria maswali haya. (Majibu ya kuandika si ya lazima)

- Hitaji kubwa sana katika kanisa langu kuhusu karama za kiroho ni nini?
- Je waumini wangu walio wengi hawajui Biblia inafundisha nini kuhusu karama zote za kiroho?
- Je karama zote za kiroho zinazotajwa katika Biblia zimo kanisani mwangu? Zipi, kama zipo, ni zipi ambazo zinadhihirika hazimo?
- Karama za kiroho zina manufaa gani kwa viongozi katika kanisa langu?
- Je nawezaje kutumia masomo katika sura hii katika kuwafundisha watu wangu kuhusu karama za kiroho?

## SURA YA 4

# MPANGO WA KUWAFUNZA VIONGOZI WATUMISHI

Sura tatu za kwanza za kijitabu hiki zimeeleza mambo makuu matatu:

1. Kuna haja kubwa ya viongozi.
2. Mtazamo wa Kibiblia juu ya uongozi ni utumishi.
3. Mungu amegawa karama za kiroho kwa kila mwamini kwa kusudi la kulijenga kanisa.

Kwa maneno mengine, Mungu ametayarisha akiba ya mahitaji kwa kiongozi katika kila kanisa. Ni juu yako kama mchungaji kuwatafuta washiriki walio na karama za uongozi na kuwasaidia wapate kutumika ipasavyo. Sura hii inashughulikia mafundisho haya manne: (1) Kutafuta watakaokuwa viongozi wa baadaye, (2) Sifa za viongozi, (3) Maisha yakiroho ya kiongozi, na (4) UongoziwaKitumishi katika matendo.

## Kuwatafuta Watakaokuwa Viongozi

Yesu alichagua na kuvuta kwake kikundi kilichoonekana hakifai kiwe viongozi wa baadaye. Wawili miongoni mwao walikuwa na moyo wa kufanya mambo haraka bila ya kufikiri hata wakapewa jina la utani "wana wa radi". Mmoja wao alikuwa mtoza ushuru wa serikali ya Kirumi, kazi iliyoonekana ya chini na ya kudharauliwa na kila Myahudi. Mwingine alishikilia sana imani yake wakati akiwa mshiriki wa kikundi cha siasa cha upinzani kilicho wania kuufuta kabisa utawala wa Kirumi. Mmojawapo alikuwa mvuvi mwenye fujo aliyekuwa na mazoea ya kusema kabla ya kufikiri. Mwingine alikuwa mwizi na msaliti. Hata hivyo, Yesu aliona katika watu hawa uwezo wa baadaye wa uongozi wa kitumishi.


Yesu hakuwaangalia wanafunzi wake kwa sifa walizokuwa nazo wakati huo, bali aliwaangalia kwa sifa ambazo wanaweza kuwa nazo baadaye. Ndani ya Simoni Petro aliona mtu kama mwamba atakayehubiri wakati wa Pentekosti. Ndani ya Mathayo aliona mwandishi wa Injili.

Na sisi pia, tuchunguze uwezo uliojificha ndani ya mtu. Kama vile mbegu ndogo ya Mkuyu inavyokuwa Mkuyu mkubwa, watu wana uwezo wa kustawi na kuwa viongozi wanaofaa. Hasa tuchunguze nini katika wale watakaokuwa viongozi? Jambo la kuchagua wale wa kufundishwa uongozi wa kitumishi liendeshweje?

Anayefaa kuwa kiongozi lazima awe mwaminifu. Lazima awe mwaminifu kwa Kristo, kwa kanisa, na kwa lengo la kuwa kiongozi mtumishi anayefaa.



| | Mara Chache | Mara kwa Mara | Kila Mara |
|---|---|---|---|
| 1. *Nguvu* - ninautunza mwili wangu kwa kupata chakulakinachofaa, pumziko, na mazoezi | 1 | 2 | 3 |
| 2. *Kukazana* - huendelea kufanya kazi hata kama kuna vipingamizi na kukatisha tamaa, si mtu wa kuiacha kazi. | 1 | 2 | 3 |
| 3. *Uhodari* - nazikabili hatari na shida kwa moyo thabiti. | 1 | 2 | 3 |
| 4. *Kukata shauri kwa busara* - hupima mambo na kuchukua hatua bila kuchelewa. | 1 | 2 | 3 |
| 5. *Tabia ya uanzishaji jambo* - mimi ni "mwanzishaji" na nina shughuli za kuwaelekeza watu waanze jambo | 1 | 2 | 3 |
| 6. *Uthabiti* - tabia ya kuwa imara ni thabiti na imara na mara nyingi sibadiliki. | 1 | 2 | 3 |
| 7. *Kujimiliki kwa nidhamu* - nina akili ya utulivu inayoamua kwa busara na hutawala vitendo vyangu na hamasa. | 1 | 2 | 3 |
| 8. *Kutokuwa na choyo* - kwa furaha huyatumia maisha kwa ajili ya wengine na hugawana mali yangu na wengine. | 1 | 2 | 3 |
| 9. *Subira* - naweza kushikilia jambo pakiwepo upinzani na naweza kuendelea hata kama mzigo umekuwa mzito. | 1 | 2 | 3 |
| 10. *Imani* - nina imani kubwa kwa Mungu. | 1 | 2 | 3 |
| 11. *Uaminifu thabiti* - ni mwaminifu tabia ya uwazi na naweza kutegemewa. | | | |
| 12. *Moyo wa utumishi* - nina utashi halisi wa kumtumikia Kristo kwa kuwatumikia wengine. | 1 | 2 | 3 |




## TAO LA UONGOZI WA KITUMISHI

Jipime maisha yako kwa kutumia sifa hizi. Jipime katika kila kipengele kwa kutumia mizani inayofuata. Tena, utahitaji kutumia mizani hii baadaye na wale unaowafunza. Chora mviringo kwa namba inayolinganisha maelezo juu ya sifa yako. Ukiwa nayo mara chache mviringo itazunguka namba 1, mara kwa mara ni namba 2; kwa kila mara weka mviringo kwa namba 3.



Awe tayari kutumika. Awe amejitoa kabisa kuwa kiongozi mtumishi kwa kiasi kwamba atatenga muda ajifunze na kujiendeleza. Awe tayari kufundishwa. Atambue wajibu wako kama mfundishaji wa kuwakamilisha na awe tayari kujifunza.

## Sifa za Viongozi Watumishi

Paulo anatoa orodha pana ya sifa za kiongozi mtumishi katika 1 Timotheo na Tito. Ingawa sifa hizi zinahusu hasa mchungaji, zinaweza kutumika kwa wale wote waliojitoa kufuata mfano wa Kristo katika kuwatumikia wengine. Sifa hizi zinatoa picha nzuri ya kiongozi mtumishi.

Soma 1 Timotheo 3:1-5 na Tito 1:5-9 katika Biblia yako. Sasa jifunze chati inayofuata. Soma kila sifa na maelezo. Halafu tumia mizani kwenye safu ya mkono wa kulia kwa kujipimia kwa kila sifa. Baadaye utahitaji kutumia chati hii pamoja na wale unaowafunza.

Chora mviringo kwa namba inayoeleza hasa jinsi sifa inayokuridhisha. Kwa mfano, ikikuridhisha sana chora mviringo kwa namba 3. Ikiwa umo katikati, chora kwa namba 2. Ikiwa hata kidogo, chora mviringo kwa namba 1. Ujipime wewe wenyewe, kwa kadiri unavyoona.

| **Sifa za Viongozi Watumishi<br>1 Timotheo 3:1-5** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Sifa | Maelezo | Ninavyoonekana Inaridhisha<br>Hata Kidogo | Mara kwa Mara | Sana |
| 1. Asiyelaumika (ms.2) | Aliye na tabia nzuri, asiye shtakiwa na watu. | 1 | 2 | 3 |
| 2. Mume wa mke mmoja (ms.2) | Mume wa mke mmoja | 1 | 2 | 3 |
| 3. Mwenye kiasi (ms.2) | Mtaratibu, mtulivu mwenye akili nzuri, akili ya utu. | 1 | 2 | 3 |
| 4. Mwenye busara (ms.2) | Anajizuia, anajimiliki, akili tulivu yenye kuamua mambo kwa | 1 | 2 | 3 |
| 5. Mwenye utaratibu (ms.2) | Maisha yenye mpango nzuri, yenye kuheshimika, anawavutia | 1 | 2 | 3 |
| 6. Mkarimu (ms.2) | Mkaribishaji wageni, anawapenda wengine, yu tayari kugawana kitu na wengine. | 1 | 2 | 3 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **7**. Anayeweza kufundisha (ms.2) | Mwenye uwezo wa kueleza Neno la Mungu kwa wengine. | 1 | 2 | 3 |
| **8**. Si wa kuzoelea ulevi (ms.3) | Hatumii kileo, hajirahusu kutawaliwa na cho chote kinachoweza kudhuru mwili wake kwa Kristo. | 1 | 2 | 3 |
| **9**. Si mtu wa matata (ms.3) | Hawapigi watu au kuwarudishii maneno ya kuwaumiza si mgomvi. | 1 | 2 | 3 |
| **10**. Mpole na mwenye amani (ms.3) | Mwenye subira, ni rahisi kushirikiana naye. | 1 | 2 | 3 |
| **11**. Asiwe wa kupenda fedha (ms.4) | Siye mpenda fedha | 1 | 2 | 3 |
| **12**. Mwenye Kuisimamia nyuma yake vema (ms.4) | Ni kiongozi mwema wa familia, familia inatabia nzuri na yenye kuheshimika. | 1 | 2 | 3 |
| **13**. Aliyekomaa katika imani (ms.6) | Si mtu aliyeongoka karibu. | 1 | 2 | 3 |
| **14**. Ashuhudiwe mema na watu walio nje ya kanisa (ms.7) | Mwakilishi mwema wa Yesu katika sehemu zote za maisha. | 1 | 2 | 3 |
| **Tito 1:5-9** | | | | |
| **15**. Asiwe mwenye majivuno (ms.7) | Asiwe mwenye majivuno; asiwe mtu mwenye kujipenda nafsi yake, si mtu amabaye kila siku anafuata yake | 1 | 2 | 3 |
| **16**. Asiwe mwepesi wa hasira (ms.7) | Hachemki kwa hasira. | 1 | 2 | 3 |
| **17**. Mpenda mema (ms.8) | Aweza kuona upande mzuri katika jambo, hutafuta mema badala ya mabaya. | 1 | 2 | 3 |
| **18**. Mwadilifu na mtakatifu (ms.8) | Kielelezo hai cha Ukristo. | 1 | 2 | 3 |



| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **19**. Mwenye nidhamu (ms.8) | Anayo mafundisho ya unyofu na mwenye kutawala nafsi yake. | 1 | 2 | 3 |
| **20**. Akilishika kikamilifu Neno (ms.9) | Mwenye utii na amejitolea kwa Neno la Mungu. | 1 | 2 | 3 |

Ni sifa gani tatu zinawakilisha sehemu ya maisha yako, ambako marekebisho zaidi yanahitajiwa? Andika sifa hizo hapa chini na karibu na kila moja andika hatua unavyoweza kuchukua kurekebisha katika sehemu hiyo.

| Ambako marekebisho yanahitajiwa | Hatua nitakayochukua |
|---|---|
| 1. ______ | 1. ______ |
| 2. ______ | 2. ______ |
| 3. ______ | 3. ______ |

Njia nyingine ya kuangalia sifa za uongozi wa kitumishi ni kuweka mkazo juu ya sifa za kimwili, kiakili na kimawazo, kijamii na kiroho zinazoonekana katika viongozi watumishi. Jifunze tabia katika mchoro unaofuata. Tumia kamusi yako kutafuta maana ya tabia yoyote ambayo si wazi kwako.